MILANGO NDANI YA MLANGO

. . . hapa asubuhi hii. Nilikuwa nikiwazia juu ya wakati wangu kuja Flagstaff ma—mara ya kwanza. Imekuwa kama, nadhani, kama miaka thelathini na minane iliyopita, labda arobaini. Nilikuwa nikizungumza kuhusu kupanda kilima. Hakukuwako na theluji, bali ilikuwa ni vigumu kwa maskini gari langu la Muundo wa T kupanda kilima. Lingeweza kwenda maili thelathini kwa saa, lakini hiyo ni kumi na tano upande *huu* na kumi na tano upande *huu*, mwajua, kwenye baadhi ya barabara hizi tulizokuwa nazo hapa. Na ilikuwa ni ninii kabisa . . .

2 [Ndugu mmoja jukwaani anasema, "Kwa nini usitukaririe lile shairi la Ford."—Mh.] Ndugu Carl! ["Tafadhali."] La. Yeye ananiambia kuhusu shairi dogo nililokuwa nalo wakati mmoja, la juu ya Ford yangu. Si mahali panapofaa pa kulikariri, Ndugu Carl.

3 Kwa hiyo, tunashukuru sana. Nami nilikuwa na shuhuda nyingi sana za kupendeza asubuhi ya leo, kusikia kutoka kwa hawa ndugu, nilikutana na baadhi ya wanaume hao.

4 Na kulikuwako na mhudumu tu ambaye ndio kwanza ahubiri hapa, maskini ndugu Mhispaniola aliyempa nanii wake . . . mvulana huyo mdogo nafasi ya kuimba. Hivi hilo halikuwa ni jambo zuri sana kwa sauti ya umri wa miaka sita? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Jamani, sauti ndogo nzuri kuliko zote nilizopata kusikia, kwa mvulana mdogo kama huyo.

5 Sasa, ndugu huyu, ndugu walisahau hilo, bali anafanya mkutano hapa mjini penu. Nafikiri ni huko kwenye church of God, ama ni Assemblies of God? [Ndugu huyo anasema, "Assemblies."] Assemblies of God, huko chini kwenye Assemblies of God. Nami nina hakika wangefurahia kuwepo kwenu—kwenu. Huo mkutano unachukua muda gani, ndugu? ["Mpaka Jumapili."] Mpaka Jumapili. ["Jumapili usiku."] Mpaka Jumapili usiku. ["Tutakuwa na uvuvio wa kuimba usiku wa leo."] Ati nini bwana? ["Tutakuwa na uvuvio wa kuimba usiku wa leo."] Uvuvio wa kuimba usiku wa leo. Sasa ninyi nyote mmealikwa kwa furaha kuhudhuria mkutano huu. ["Kwenye saa moja na nusu."] Saa moja na nusu, usiku wa leo. Na kanisa hilo liko wapi, ndugu? ["Mtaa wa 113 wa West Clay."] Je, unaweza kutuambia tu mahali lilipo? ["Mtaa wa 113 wa West Clay."] Mtaa wa 113 wa West Clay, mumu humu katika mji wa Flagstaff. Na—na nina hakika mtaninii . . .

6 Je! mvulana huyo mdogo yuko pamoja nawe? [Ndugu huyo anasema, "La."—Mh.] La, baba yake ataimba. Wewe huimba, sivyo? Vema, hilo ni sawa, ninalipata hilo vizuri tu, kwa mara ya kwanza. Vema, hilo huonekana kwa nadra sana; lakini ni ninii,

kwa kawaida, kama kuna kipaji kimoja katika familia, we—wengine wanakipata, nafikiri. Kwa hiyo wananinii. . . [“Yote yalianza kwa kufunga na kuomba, Ndugu Branham.”] Kufunga na kuomba, sasa hilo—hilo ni zuri kweli.

7 Sasa, unajua, kama Marekani, wote pamoja, familia zetu zote za Marekani zingelikuwa hivyo, vema, wangekifuta kazi kikosi chote cha polisi. Ule Utawala wa Miaka Elfu ungeanza, sivyo? Tungekuwa moja kwa moja kwenye tabaka la kwanza basi. Hiyo ni kweli. Kifo chote kingetoweka, maradhi yote, huzuni, maudhi yote, nasi tungekuwa pamoja na Kristo.

8 Kwa hiyo, tuna furaha, nami ninasikia shuhuda hizi zote nzuri! Na nilikuwa na majaliwa ya kukutana na Ndugu Earl, kwa mara yangu ya kwanza. Na—na jana jioni nilikuwa nikizungumza na mke wake, na—naye alikuwa ameitwa na kuponywa, mara nyingi, mikutanoni; kasema, kwenye ule mkutano wa mwisho alikuwa jukwaani.

9 Kwa hiyo, linatufanya ninii kidogo, kwa namna fulani ucheshi mdogo. Sikumkumbuka Ndugu Earl, ingawa nilikuwa nimempa mkono mahali fulani. Na—nami nilikuwa nimeketi kwenye dirisha, jana usiku, nikimtarajia aje. Ndipo mtu mrefu sana akaingia, alikuwa na masharubu meusi. Nikasema, “Huyu hapa anakuja.” Na halafu wakati. . . Billy, mwanangu, akasema, “Loo, la,” kasema, “huyo si Ndugu Earl. Yeye ana umri mdogo zaidi kuliko jamaa huyo.” Na ndipo basi nikaweza kukutana na Dada Earl hapa jana jioni, nami nilikuwa na majaliwa ya kuwa kwenye nyumba yao inayopendeza hapa mjini.

10 Hapa ni mahali pazuri. Daima nimependa kupaita *flagpole* badala ya Flagstaff, mbali sana juu ya kilima hapa, mnaona. Na, nawaambia, kama kuna mtu yeyote hapa kutoka Texas, sasa mnajigamba. Niliondoka Tucson, jana, yapata sabini na mbili ama sabini na tano, kitu kama hicho, nami niko hapa asubuhi ya leo nimevaa kabuti. Mnaona, kile walicho nacho huko Texas, tunacho Arizona, sivyo? Hiyo ni kweli. Tupo papa hapa.

11 Wakati huu wa ushirika! Mzee Daktari Bosworth, rafiki yangu, wengi wenu huenda mlimjua Ndugu Bosworth. Alikuwa ni mmoja wa wazee walio watakatifu sana. Naye aliniambia wakati mmoja, akasema, “Ndugu Branham, je! unajua *ushirika* ni nini?”

Nikasema, “Nafikiri najua, Ndugu Bosworth.”

12 Kasema, “Ni watu wawili katika meli moja, kwa hiyo inawalazimu kushiriki kidogo.”

13 Kwa hiyo hiyo ndiyo maana ya ushirika, tunatwaa na kutoa, tunashiriki sisi kwa sisi; pamoja na Ndugu Carl Williams, wengine wote, Ndugu Outlaw. Loo, mmoja wa watu wa kwanza Arizona waliopata kudhamini mmoja wa mikutano yangu, alikuwa ni Ndugu Jimmy Outlaw, nasi tumekuwa ndugu wasiri tangu wakati huo. Nasi tunafurahi sana kwa ajili yenu nyote,

kwa ajili ya wahudumu na ndugu tunaokutana nao mahali hapa. Sina wakati wa kupeana mikono na kila mtu, kama ninavyopenda kufanya, bali ni ushirika ambapo tunakutanika pamoja.

14 Inanikumbusha tu juu ya—juu ya mkutano wa Phoenix. Nimekuwa na majaliwa, tangu matawi hayo yaanze, ku—kusaidia kuyaweka katika utaratibu matawi na kuyahubiria. Na ndilo shirika la pekee ambapo mimi ni mwanachama, wala si dhehebu. Ni shirika tu linalofanya kazi miongoni mwa watu.

15 Na kama baadhi yenu ninyi wanaume hapa asubuhi ya leo, wa—wasio wanachama wa ushirika huu, wa Wafanya Biashara Wakristo, Full Gospel, hebu. . .kama mnaamini na mtachukua neno langu, ni moja la makundi mazuri sana ya watu. Na—na kwa ndugu wahudumu, halilipingi kanisa lako, linaliunga mkono kanisa lako. Unaona, ni njia yao ya kuweka ka—kanisani.

16 Imetokea tu kwamba nimeangalia huku kwenye huyu mama mzuri hapa ambaye ndiyo kwanza aimbe ule wimbo dakika chache zilizopita. Nimesikia majaribio mengi ya huo, bali mama huyo alikuwa na sauti ambayo iliuimba vizuri, mwajua, bila ya kuuimba kwa sauti nyembamba, kitu kama hicho. Niliupenda huo sana, mama, ulikuwa ni mzuri, mzuri sana. Ilisemekana alikuwa ni mke wa mhudumu hapa. Na, ndugu, inakupasa kumfanya akuimbie upate kulala kila usiku, kwa hiyo hilo lingekuwa ni zuri sana, zuri sana. Ulikuwa ni uimbaji mzuri sana. Niliufurahia.

17 Na, asubuhi ya leo, kwa namna fulani inanikumbusha juu ya hadithi ndo—ndogo. Kwamba, na—napenda kuwinda na kuvua samaki, na hiyo ndiyo moja ya sababu niko hapa Arizona, ili, ni kusudi nipate kuwinda na kuvua samaki. Nami napenda hilo. Na kwa hiyo nilikuwa nikivua samaki wakati mmoja huko New Hampshire.

18 Nami nadhani nina wenzangu wengi sana hapa wanaopenda kuvua samaki, wanaume kwa wanawake, pia, mnaona. Sote tunapenda kufanya hivyo.

19 Kwa hiyo nilikuwa na hema dogo la watu wawili nililokuwa nimepandisha juu sana, juu ambapo, mnajua jamaa hao, kwa namna fulani ni wazito ama kitu kama hicho, wasingeweza kupanda juu kule. Na kulikuwa na wengi wazuri, wa hao, samaki wa vijitoni, na wa hudhurungi, mkia mraba, wa maji baridi. Loo, wamejaa tu mle, hivyo vijito vidogo vikishuka kuja kutoka kwenye vilele vya milima huko New Hampshire. Nao samaki wadogo wa maji baridi, wenye urefu wa labda inchi kumi na nne, kumi na sita, wengi wao tu! Nami ningeninii tu. . .Ningeenda kule na kuwavua, kwa raha tu ya kuwavua, nawaachilia. Kama nilimwua mmoja, basi ni—ninamla huyo, mnaona, ninamwingiza ndani.

20 Kwa hiyo nilikuwa na baadhi ya miti hii myembamba ya mtoni ikikua, na—na kila wakati ningevurumisha ugwe wangu wa kuvulia . . . Nilikuwa na Inzi Chambo Bandia chache. Ningeutupa mle ndani nazo, ningeuvurumisha kwenye lundo la miti myembamba ya mtoni. Nami nikawazia, "Vema, nitachukua kishoka na kupanda kule, asubuhi ya leo, na—na kukata miti hiyo myembamba ya mtoni, kusudi isiushike ugwe wangu." Loo, nikaangalia nyuma chini ya maskini ninii kidogo . . . kama bwawa la buku, nao walikuwa wamelala tu pale, wakingojea tu hicho chambo kiwashike. Sasa, usiku kucha . . . Nilizoea kusema, "wameshika nywele zangu," bali sina nywele za kutosha kwao kuingia ndani yake sasa. Kwa hiyo nilikuwa . . . Nilinii tu . . . wao jinsi tu wanavyo—jinsi wangewaangalia. Na kwa hiyo nikapanda kule, asubuhi hiyo, nikachukua maskini kishoka hiki kidogo, na kukata miti hii myembamba. Nami nilikuwa na watatu ama wanne, nilikuwa nikienda kuwapika kwa ajili ya kiamshakinywa, kisha nirudi. Nami si mpishi mzuri sana. Na kwa hiyo nilimwambia mke wangu nisingeweza kuchemsha maji pasipo kuyaunguza, kwa hiyo mnajua hiyo ingekuwa ni kazi mbaya sana ya kupika.

21 Kwa hiyo, nikiwa njiani narudi, kulikuwako na maskini mama dubu na watoto wawili, nao walikuwa wameingia kwenye hema langu dogo. Na hebu nena juu ya kuvuruga kitu, hujui jinsi vitu vingeweza kuvurugwa mpaka umwache dubu aingie hemani. Yeye, si yale wanayoharibu . . . namaanisha, yale wanayokula, ni yale wanayoharibu. Nilikuwa na stovu ndogo, hii stovu ndogo ya mchunga-kondoo mle ndani, na wangepanda juu ya stovu hii ndogo na kuruka-ruka tu juu chini, wapate kusikia paipu ikichacharika, na kuipondaponda tu vipandevipande, mwajua. Ndipo wakati nilipokuja pale, nilikuwa na maskini bunduki aina ya ishirini na mbili ya siku nyingi iliyoingia kutu imewekwa pale, bali nilikuwa na shoka hili mkononi mwangu.

22 Na, mwajua, wakati nilipokaribia, maskini mama huyo akakimbia upande mmoja, naye akawaita watoto wake. Ndipo mtoto mmoja akafuata, vyema; bali huyo mwingine akaketi, jamaa mdogo sana. Katika Mei, mwajua, ndio kwanza azaliwe. Alikuwa ameukunja mgongo wake kunielekea, namna *hiyo*. Nami nikawaza, "Kwani anafanya nini?" Vema, ndipo akaniangalia. Nami nikautafuta mti, nione jinsi—jinsi ulivyokuwa karibu, maana wanaweza kukupiga kucha, unajua, kuhusu watoto hao. Na, wao, huwezi kuwashawishi waachane nayo, unaona. Kwa hiyo nikamwangalia maskini mama huyo kwa muda kidogo, wajua. Aliendelea kuita, na kupiga kelele, kitu kama ndege. Ingekubidi kujua jinsi moja inavyosikika. Kwa hiyo akaendelea kumwita mtoto huyo mchanga, na mtoto huyo asingekuja.

23 Vema, nikawaza kuhusu bunduki yangu. Nami nikawaza, "La, kama ningekimbia niingie mle ndani na kuinyakua hiyo

bunduki, kama ningempiga risasi maskini mama huyo, niwaache mayatima wawili mwituni," wala sikutaka kuwa na hatia ya jambo hilo. Na, mbali na hayo, yeye akishambulia, hiyo ya ishirini na mbili kwa namna fulani ingekuwa ni ndogo, unajua. Na wakati mwingine haikufyatuka, huna budi kuikonyoa mara tatu ama nne kuifanya ifyatuke. Kwa hiyo nikawazia, "Vema, nitapanda tu kwenye mti ule pale, akielekea huku. Nitapanda kule juu mtini, nijitafutie kiboko kidogo na kuwatwanga tu puani." Pua yao ni nyororo sana. Nao wanalia tu, kisha wanaanguka, unajua, nao wanakuacha. Kwa hiyo nikawazia, "Nitapanda kwenye mti ule."

24 Lakini udadisi wa maskini jamaa huyo mdogo, loo, ameketi namna *hii*. Ndipo nikawaza, "Anafanya nini?" Kwa hiyo nikaendelea kunyemelea pale, nikimwangalia, wajua, nikizidi kwenda mbali, na kuukaribia ule mti, maana aliendelea kumwita yule mtoto. Kwa hiyo nikafika mbali kidogo, nanyi mnajua kile maskini jamaa huyo mdogo alichokuwa amefanya?

25 Sasa, ninapenda keki za magole, ama chapati za maji, ninaamini ndivyo mnavyoviita, huku. Huko Kusini, tunaviita keki za magole. Nami si mjuzi sana kwa kuzipika, bali hakika ninapenda sana kuzila. Na, mwajua, nilikuwa Mbaptisti. Sipendi kunyunyizia; kweli ninapenda kuzibatiza, kuzitumbukiza kwelikweli katika 'lasi. Kwa hiyo nilikuwa na kopo la molasi, kubwa *hivi*, limewekwa pale, ndoo ya nusu galoni kwa ajili ya magole yangu.

26 Na maskini jamaa huyo, unajua, dubu anapenda kitu kitamu, hata hivyo. Alikuwa ameifunua hiyo ndoo ya molasi. Naye alikuwa ameketi pale na wayo huo mdogo wenye upana kama *huu*. Naye alikuwa ameishika kwa mikono yake, naye alikuwa tu akiutumbukiza mguu wake mdogo ndani, na kuulamba namna *hiyo*, unajua. Hiyo ni kweli. Naye angeramba maskini ulimi huo mdogo. Nami nikaanza... Na laiti ningalikuwa na kamera, ningalipenda kuonyesha jambo hilo asubuhi ya leo, kuliangalia tu. Na huyo hapo, akiutumbukiza mguu wake mdogo pale, na kuuramba namna *hiyo*. Nami nikapaza sauti, "Ondoka hapo," namna hiyo. Wala hakunijali hata kidogo, na akaendelea tu kuramba namna hiyo. Aliiilowanisha ndoo hiyo kabisa, unaona.

27 Nami nikampigia kelele namna hiyo, akageuka na kuniangalia namna *hiyo*. Asingeweza kuyafungua macho yake, alikuwa amefunikwa na molasi kabisa, unajua. Kote machoni mwake, maskini tumbo lake dogo, limejaa tu molasi alivyoweza kujaa! Halafu basi, baada ya kitambo kidogo, akayumbayumba upande mmoja, akamkimbilia tu mamaye. Walimpeleka huko kichakani wakaanza kumramba. Waliogopa kuketi kwenye ile ndoo, bali wangeweza kumramba.

28 Nami nikasema, “Kama huo si mfano wa mkutano mzuri wa kale wa kipentekoste; unajaa tu vitu vizuri, vitamu, wanatoka kwenda huko nje, naye mtu mwingine anamramba. Huo ni mkutano halisi wa ushirika. Sasa sisi tunakuja tu namna hii, tupate kuingiza mikono yetu kwenye ndoo, kila mmoja wetu, kufikia kwenye kiwiko, kwenye baraka za Mungu. Nami nina hakika mtapata hayo kwenye mkutano ulio huko chini kwenye Assemblies of God, unaoendelea kule chini sasa. Bwana awabariki.

29 Nilisema huko Phoenix, hivi majuzi, ninii kidogo... Natumaini halikusikika la kukufuru, kuhusu ucheshi mdogo kuhusu mhudumu ambaye angeenda jukwaani kila asubuhi, kwa muda wa miaka ishirini, imara, angehubiri dakika ishirini, na basi amemaliza, na kwa hiyo wasingeweza kuelewa ni kwa nini ilikuwa hivyo. Na kwa hiyo, asubuhi moja, alihubiri kama saa nne. Ndipo ma—mashemasi wakamwita, na—na wakasema, “Mchungaji, kweli tunakupenda.” Kasema, “Tu—tunafikiri jumbe zako ni nzuri sana.” Kisha kasema, “Tunajua, kama halmashauri ya mashemasi, tumekuangalia na kukupimia wakati, dakika ishirini kamili kila Jumapili asubuhi.” Kisha wakasema, “Asubuhi ya leo ilikuwa ni saa nne.” Wakasema, “Hatuelewi kabisa.”

30 Kasema, “Nitaawaambia, ndugu.” Akasema, “Kila asubuhi, ninapoenda kuhubiri,” kasema, “mnaponialika jukwaani, ninachukua mfukoni hizi peremende za Okoa Maisha na kuziweka chini ya ulimi wangu. Na,” akasema, “katika dakika ishirini, wakati hiyo Okoa Maisha imekwisha,” kasema, “Mimi—mimi—mimi nimemaliza,” akasema, “Ninajua wakati wa kumalizia umefika.” Kisha kasema, “Kosa lililotokea asubuhi ya leo, nilichukua kifungo.”

31 Carl Williams, Jewel Rose, ndugu na marafiki wasiri wangu halisi, walishuka mjini hivi majuzi, nao wakachukua kifungo chenye ukubwa namna *hii*, wapate kunipa, na, bali sinacho asubuhi ya leo. Kwa hiyo, tunashukuru kuwa hapa.

32 Sasa, kuna yeyote hapa anayemfahamu Daktari Lee Vayle? Sidhani...labda hamna. Yeye alikuwa mhubiri Mbaptisti, Daktari wa Uungu, naye ana digrii zake. Yeye alikuwa ni mwalimu wa shule ya sekondari ya juu, kwanza, naye ni mtu mzuri sana, msomi. Na kanda zangu za *Nyakati Saba Za Kanisa*, nilizituma kwake, apate kuziweka katika sarufi. Kwa sababu, Kikentaki changu cha “tio, abana, na tote, na beba, tafuta,” hicho hakiendani vizuri na watu wanaovisoma vitabu hivyo, kwa hiyo alikuwa aniwekee hicho sarufi. Halafu basi, baada ya yeye kumaliza, akakirudisha mara kadhaa, kwa ajili ya maelezo zaidi. Ambapo, kitabu hicho kinaingia kwenye mtambo wa kuchapisha sasa, baada ya kama miaka mitatu ama minne.

33 Yeye aliniuliza, akasema, "Ninaweza kuandika kitabu, maoni yangu tu?"

Nami nikasema, "Vema, ni sawa, Ndugu Lee." Basi nikawazia . . .

34 Kisha akasema, "Nitakwambia jambo fulani." Kasema, "Hakitauzwa; ni cha kutolewa bure."

Nikasema, "Vema, basi, nina hakika hilo ni sawa." Unaona?

35 Na kwa hiyo walikuwa na udhamini, wa karibu watu kumi kukidhamini, ambacho kiliwagharimu karibu dola elfu moja na mia tano, nafikiri, nasikia, kwa nakala elfu kumi. Na kwa hiyo tu—tunavyo, vyote vilitoka mitamboni siku kadhaa zilizopita, nasi tukapewa viwili ama vitatu, jana, na Billy alivileta. Navyo vi—vinatolewa bure. Sasa, kamwe sijakisoma, sijui alichosema. Lakini ninaninii . . . Hii ni kwa imani. Lakini nina hakika, kama ukitaka kupata kimoja, kama ukituandikia tu, kitatumwa kwako, bure. Mnaona? Nacho kinaitwa *Nabii Wa Karne Ya Ishirini*.

36 Na halafu nikaona kwenye picha hapa, kwenye jalada mbele ya kitabu, wengi wenu mna picha hii, bila shaka, na mmeiona, hapo ndipo Malaika wa Bwana alipigwa picha huko Houston, Texas. Bali walikatilia mbali sehemu Yake.

37 Kisha ninaona hapa upande wa nyuma. Na ni wangapi hapa wamekuwa katika mmoja wa mikutano hiyo, hebu tuone? Nadhani ni karibu ninyi nyote mmehudhuria. Mnanisikia nikisema, mara nyingi, "Hicho kivuli kinaning'inia juu ya mtu fulani." Sasa, mnaona, kama ukitoa tamshi, na si la kweli, Mungu hatakuwa na uhusiano wowote nalo. Unajua Mungu hahusiki katika uongo, bali yeye hutetea tu yaliyo kweli.

38 Kwa hiyo wakati alipomwambia Musa, wakati alipokutana naye kule nyuma nyikani, katika ile Nguzo ya Moto, kule nyuma kwenye kile kichaka kilichowaka moto. Ndipo wakati alipowatoa watu hao, na wale ambao wangemfuata Musa wakitoka, kwa ajili ya safari, basi alishuka juu ya Mlima Sinai, Nguzo hiyo hiyo ya Moto, na kuthibitisha ya kwamba kile Musa alichokuwa amesema kilikuwa ni kweli.

39 Sasa, Mungu atafanya jambo hilo. Daima hufanya hivyo. Kwa hiyo Nuru hii *hapa*, bila shaka, tunaihusisha na Mungu, kwa maana ina tabia ile ile na kila kitu alichofanya wakati alipokuwa hapa duniani.

40 Halafu juu ya hilo, kusema, "Mtu huyu hapa, ninaona umetiwa uvuli wa mauti, kivuli cheusi." Ni wangapi, wengi wenu mmesikia hilo likisemwa! Vema, hapa hivi karibuni tu mkutanoni, kulikuwako na mtu fulani mdadisi, aliyetaka kuona kama wangepata picha ya hicho, wakati iliposemwa. Kwa hiyo wao . . . Kulikuwako na mama fulani aliyekuwa ameketi hapo karibu, naye mtu huyu alikuwa na kamera. Ndipo

nikasema, "Bibi huyu anayeketi hapa, ni Bibi *Nanii*," yeyote yule. Nikasema, "Ametiwa uvuli wa mauti, bali ana kansa." Na papo hapo akapiga picha, maana ilikuwa ni hapo karibu. Na hiyo hapo, mnaona, hiyo kansa nyeusi iliyomfunika, ya mauti, ikining'inia juu ya mwanamke huyo. Ndipo Roho Mtakatifu akazungumza tena . . .

41 Sasa, wakati walipoiweka hii kwenye kitabu, walikuwa wameikata, kwa hiyo wameiweka hii hapa ndani mpaka tu watakapokichapisha kitabu mara nyingine. Na hiyo ndiyo sababu mtauona ukurasa huo usiounganishwa humo ndani. Nafikiri *Sauti Ya Uponyaji* ndio waliokichapisha kitabu hiki.

42 Na sasa kinatolewa bure kabisa. Na wadhamini hapa nyuma ya kitabu, ambao waliweka dola elfu moja mia tano katika jambo hilo, wapate tu kukisambaza kwa umma, kuuacha umma uvisome. Kwa hiyo, hakiuzwi, na ni kitabu kidogo kizuri. Na mimi sijui yaliyomo, sijakisoma kamwe; Baba anajua hilo.

43 Lakini mnaona, kilikuwa, kwangu mimi, ni Kweli kabisa. Hiyo ndiyo tunayotafuta, ni Kweli. Yesu alisema, "Mtaijua Kweli, Kweli itawaweka huru." Naye ni Kweli hiyo. Yeye ni, Yesu, Mwana wa Mungu, Ndiye Kweli ya Neno, kwa maana Yeye alikuwa ni Neno lililofanyika mwili. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Basi, hilo lilimfanya ile Kweli, kwa sababu Neno ndilo Kweli, Naye alikuwa hiyo Kweli.

44 Sasa wakati tunapomwona akirudi katika siku hizi za mwisho, huduma hii kubwa ya Mungu, akipitia kwenye mataifa ya ulimwengu, akiwakusanya watu kwa ajili ya Bibi-arusi, hiyo ni Kweli.

45 Miaka kadhaa iliyopita, wao walisema, "Hakukuwako na kitu kama kunena kwa lugha. Ilikuwa ni upuuzi." Mungu aliahidi jambo hilo, Naye akalithibitisha hilo kwamba ni Kweli. Hiyo ni kweli.

46 Mtu fulani alisema, asubuhi ya leo, ninaamini ilikuwa ni dada yetu mwadilifu pale ambaye hushughulika sana na watoto kuhusu ubatizo wao, alisema, "Unaweza kumsikia mtu fulani akinena kwa lugha. Lakini, kumsikia mtu akiimba katika lugha, unaona, lilikuwa ni jambo la kupendeza sana."

47 Ninakumbuka tukio langu la kwanza nilikuwa kwenye Maskani ya Rediger huko Fort Wayne, Indiana. Nami nilikuwa nikihubiri, nikifanya ibada ya uponyaji, baada ya kifo cha—cha Ndugu B. E. Rediger. Na Ndugu Bosworth alikuwapo, Paul Rader. Na wengi wenu ninyi mlio na umri mkubwa zaidi, kama mimi, mnamkumbuka Paul Rader; na alikuwa ni Mbaptisti, nasi tulikuwa hivyo pia, kwa hiyo tulikuwa marafiki wasiri. Na kwa hiyo wakati tukihubiri pale, nilikuwa nikienda kuwaombea wagonjwa. Lilikuwa ni jambo la kigeni kwao wakati huo. Lakini

mama mmoja alimleta mvulana mdogo pale, ambaye alikuwa amelemaa, na, wakati akija jukwaani, ono la Bwana lilitokea na kumwambia yote kuhusu kilichokuwa ni shida ya mtoto huyo mdogo. Ndipo nikamwomba msichana huyo anipe—anipe mvulana huyo mdogo.

48 Sasa kwa ajili tu ya ushuhuda wa huyo dada, mpate kuona ni furaha jinsi gani na ni tukio halisi jinsi gani la—la neema ya Mungu, yale ingeweza kufanya, wakati ikitenda kazi kulingana na Neno la Mungu, mnaona, ahadi ya Mungu kwa ajili ya wakati huo.

49 Sasa, ahadi ya Mungu kwa Nuhu haitafanya kazi kwetu siku hizi. Ahadi ya Mungu kwa—kwa Musa, tusingeweza kuwa na Ujumbe wa Musa. Musa asingeweza kuwa na ujumbe wa Nuhu. Sisi tuna Ujumbe wa wakati huu. Tusingeliweza kuwa na ujumbe wa Luther. Tusingeliweza kuwa na ujumbe wa Wesley. Huu ni wakati mwingine. Mungu aliligawa Neno Lake kwa kila wakati. Na hapo wakati huo unapotokea, Yeye humtuma mtu fulani hapo kuthibitisha Neno hilo, kuthibitisha kwamba hiyo ni kweli. Na sasa tunaona katika kila mmoja basi, kama tu vile Yesu alivyosema alipokuwa duniani, Yeye alisema, "Mnayajenga makaburi ya manabii, na baba zenu ndio waliowaweka mle."

50 Sasa, watu wangu ni Wakatoliki, kama mjuavyo, nikiwa ni Mwairishi. Sasa sisi. . . Sasa wao—wao wanazungumza juu ya Mtakatifu Patrick, Wakatoliki wanamdai. Vema, yeye ni Mkatoliki tu kadiri nilivyo mimi. Wanazungumza juu ya Joan wa Arc. Walimchoma moto msichana huyo kwenye nguzo, kama mchawi, sote tunajua hilo, kwa kuwa alikuwa ni wa kiroho na aliona maono. Bila shaka, miaka mia kadhaa baadaye, waliichimbua miili ya makasisi hao, na kufanya vitubio, na wakaitupa mtoni. Lakini hilo silo linalohitajika, unaona.

51 Daima wanalikosa. Mwanadamu daima anamsifu Mungu kwa yale aliyofanya, akitazamia yale atakayokuwa, na kupuuza yale anayofanya. Hiyo ni tabia tu ya mwanadamu. Wala hajabadilisha tabia yake, mwanadamu wa ulimwenguni.

52 Kwa hiyo tunaona ya kwamba Ujumbe wetu ni, siku hizi, Ujumbe tulio nao, wa, "Tokeni Babeli, na mwe huru, na—na mjazwe na Roho, na taa zenu zitengenezwe na kusafishwa, na, mwangalie juu, ukombozi wetu unakaribia," mambo haya ni ya kigeni kwa watu wengi ambao wanalipumua na kuliitia Jina la kupendeza la Bwana wetu.

53 Lakini hata hivyo katikati ya hayo yote, hatuna lolote dhidi ya watu hao, hao watu wa kimadhehebu. Wao wako sawa, ni wazuri. Wao ni ninii yetu—wao ni wenzetu katika Injili, kwa kuwa Yesu alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na—na wote alionipa Baba, watakuja."

54 Kwa hiyo, sisi tunawajibika tu kwa kuzipanda Mbegu. Baadhi zilianguka kando ya njia, baadhi kwenye udongo wa aina mbalimbali, baadhi zilianguka na zikazaa mara mia. Kwa hiyo, sisi ni wapanda Mbegu tu. Mungu Ndiye anayeiongoza wakati inapoanguka. Na sasa tunaomba ya kwamba labda, asubuhi ya leo, kutakuwa na Mbegu ndogo itakayoanguka mahali fulani, ambayo huenda ikamtia mtu fulani moyo. Na kama tu mwa—mwa—mwanadamu . . .

55 Kumalizia ushuhuda wangu juu ya maskini mama yule niliyekuwa ninene habari zake. Mama huyu alimleta maskini mtoto huyu mchanga, mvulana mdogo, nadhani, mwenye umri wa karibu miaka kumi, kumi na miwili, na labda hajafikia umri huo, maana mwanamke huyu alikuwa amembeba. Naye akamkabidhi kwangu. Na mara tu, wakati nilipokuwa nikimwombea mtoto huyo, jamaa huyo mdogo akaruka kutoka mikononi mwangu na akatimua mbio jukwaani, lenye kadiri ya watu elfu tatu mia tano ama elfu nne. Na walipofanya hivyo, jambo la kwanza walilopata kuona likitendeka, mama huyo, akiketi kwenye kiti cha mbele, alizimia tu na kuanguka chini. Na maskini msichana mdogo wa Kiamishi . . .

56 Hivi mnawafahamu Waamishi? Sijui kama mnao huku, nywele ndefu, hao ni watu wazuri sana, na ni watu safi na wazuri. Mwajua, katika Wamenoni wote, ama Waamishi, na kadhalika, hatuna taarifa hata moja ya uhalifu wa vijana. Waiteni ni watu wa kuchekesha mkitaka, bali sisi—sisi tuna kasoro ya jambo fulani nyumbani mwetu, ambalo wanalo. Hawana taarifa hata moja kwenye mahakama, ya—ya tabia mbaya ya watoto inayotokea miongoni mwao. Wanawalea watoto wao, kwa njia moja tu, na hiyo ndiyo njia wanayoifuata.

57 Basi msichana huyu alikuwa ni mpiga piano mashuhuri, msichana mrembo, na nywele ndefu, za rangi ya shaba zilizofungiwa nyuma. Na alipoangalia upande wa pili . . . Sasa, yeye alikuwa ni Mwamishi, hakujua kitu chochote kuhusu Pentekoste, wala mimi. Lakini wakati alipoangalia upande wa pili wa jukwaa, na kumwona mvulana huyo mdogo akienda, akitembea pale, aliitupa mikono yake hewani.

58 Sasa, ninajua kuna ushupavu wa dini, nami ninatumaini sielekei huko. Mi—mimi si mdanganyifu. Nami si—sivyo nilivyo. Kama nimekosea, si—sijakosea makusudi, nimekosea kwa kutokujua.

59 Lakini msichana huyo aliitupa mikono yake hewani, nazo nywele hizo zikaanguka kwenye mabega yake, na akaanza kuimba katika lugha ngeni. Naye alikuwa akiuimba wimbo huo, "Yule Tabibu Mkuu yu karibu sasa, Yesu mwenye huruma." Na wakati aliporuka juu kutoka hapo . . . Ninajua hili linasikika ni la kigeni sana sasa. Lakini msichana huyu kamwe hakuwa amejua kitu kuhusu kunena kwa lugha, lakini alikuwa akiimba

katika lugha ya kigeni. "Yule Tabibu Mkuu yu karibu sasa, Yesu mwenye huruma." Na hiyo piano ikaendelea kucheza, "Yule Tabibu Mkuu yu karibu sasa, Yesu mwenye huruma." Vema, walisongamana kwenye madhabahu, na kote kupitia roshani, hata sakafuni, watu wakipiga makelele! Msichana huyo akisimama pale, ameinua uso wake juu namna *hiyo*, akinena kwa lugha zingine, na, hiyo piano, hivyo vibao vyenye rangi ya vipusa vya ndovu vingali vikicheza:

> Yule Tabibu Mkuu yu karibu sasa,
> Yesu mwenye huruma,
> Yeye hunena kuchangamsha mioyo yenye huzuni,
> Hakuna Jina jingine ila Yesu!

60 Loo! Ni. . . "Jicho halijapata kuona, wala sikio kusikia, yale tuliyowekewa akiba." Mnajua yale ninayowazia? Kwa nini— kwa nini tukubali kibadala ama kitu ambacho ni kujifanya kuamini, wakati mbingu zimejaa kilicho halisi, Nguvu halisi za Mungu, ambazo zinaweza kuiweka nafsi huru, ambazo zinaweza kutufanyia jambo fulani? Mungu awabariki. Sasa, kuna mambo mengi sana.

61 Sikuwaambia mahali pa kukipata kitabu hiki, mnaona. Sanduku la Posta 325, huko Jeffersonville. Na kama ungeandika, mbona, wangekutumia. Ama, au, uhudhurie moja ya mikutano hii, watakuwa wakivigawa.

62 Sasa, ninashukuru sana kwa wakati huu mzuri wa ushirika. Na asubuhi ya leo nilikuwa nikiwazia juu ya hadithi ndogo niliyokuwa nikisimulia kwenye Wafanya Biashara Wakristo, kuhusu Zakayo. Wengi wenu mmenisikia nikiisimulia, jinsi ambavyo maskini jamaa huyu hakuamini katika utambuzi huu, na, wa Bwana. Hakika, nadhani, kama tulivyo nalo katika kila wakati, unamwona aliye halisi, kisha unamwona mwigaji. Nasi hatuna budi kuvumilia jambo hilo. Walakini watu wazuri wenye mawazo thabiti na wa Kimaandiko wanafahamu, unaona. Ambapo, sisi, na haidhuru . . .

63 Wakati Bibi Aimee Semple McPherson, wakati alipokuwa hapa duniani, katika huduma yake, wanasema ya kwamba karibu kila mwanamke mhubiri alivaa hizo zilizo kama mabawa, kitu kama hicho, mnajua, ama majoho kama hayo, na kuibeba Biblia.

64 Hebu waangalie tu wa akina Billy Graham walioko nchini siku hizi. Lakini, unajua, Billy Graham kamwe asingeweza kupachukua mahali pako. Nisingeweza kupachukua mahali pa Billy, asingeweza kupachukua pangu. Siwezi kupachukua pako, wala wewe huwezi kupachukua pangu. Wewe ni mtu binafsi, katika Mungu. Mungu alikufanya jinsi ulivyo, kwa kusudi fulani. Laiti tungaliweza kupajua mahali petu, na kisha kudumu pale. Kama tukijaribu kufanya jambo fulani tofauti, basi, unaona,

tuko—tuko kwenye eneo la mtu mwingine, ambapo tunaivuruga tu picha ya Mungu.

65 Tunachukua kwa mfano Billy Graham katika ulimwengu wa kimadhehebu siku hizi, kama jinsi alivyo, kama tungeliita labda kwa mchezaji wa soka, yeye ana mpira.

66 Sasa kama ukijaribu kumnyang'anya mtu wenu mpira, unaivuruga tu timu yenu. Mlindeni mtu wenu, unaona. Endeleeni kumlinda, wazuieni hao wengine kusudi aweze kutimua mbio. Nasi tutapata goli baada ya kitambo kidogo, na Yesu atakuja, ndipo yote yatakwisha. Bwana awabariki.

67 Sasa nitayaendea matamshi ya mtu huyu, Zakayo. Nami nilikuwa nimemweka juu ya mti huu, mwajua, huku amejifunika kabisa kwa majani. Na ndipo basi wakati aliposhuka kutoka kwenye mti huo, alienda nyumbani pamoja na Yesu. Ndipo nikasema, "Akawa mwanachama wa tawi la Wafanya Biashara Wakristo wa Full Gospel." Kwa hiyo kama kuna akina Zakayo wowote hapa, asubuhi ya leo, natumaini ya kwamba utachukua ushauri huo mzuri na uwe mwanachama wa Wafanya Biashara wa Full Gospel.

Unasema, "Ati Full Gospel?" Naam, bwana.

68 Huko ndiko mahali tu ambako Yesu angalihubiri, kungekuwa ni kwenye Injili yote. Hiyo ni kweli. Hiyo si ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Injili yote. Hiyo ni kweli. Yeye asingejikana.

69 Lakini sasa nina Maandiko machache yaliyoandikwa hapa, ya fungu dogo, la kawaida, halitanichukua ila dakika chache tu, kama mtanivumilia. Na kabla hatujafanya jambo hili . . . Sasa, katika ushirika wetu mdogo wa kukusanyika pamoja, na kuzungumza juu ya mikono ya dubu, katika ile ndoo, na kadhalika, sasa hebu na tuondolee mbali haya yote sasa, na kuwazia tu ya kwamba tunaendelea kufahamiana. Na, na tunataka sasa kuingia kwenye sehemu ya kilindi ya Neno.

70 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa, tunapolikaribia. Kwa maana, hatuna haki ya kulikaribia Neno, bila ya kuzungumza na Mwandishi, kwanza.

71 Huku tumeinamisha vichwa vyetu, macho yetu yamefumbwa, na ninaamini kwamba mioyo yetu imeinamishwa pamoja na vichwa vyetu. Sijui, wakati nikiinua macho yangu na kuwaangalia wasikilizaji, kama kungekuwako na mtu hapa angesema, katika kuinua mikono yao, "Ndugu, mhudumu, nikumbuke katika maombi. Mimi ni—mimi ni mhitaji leo"? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Sasa Yeye anauona mkono wako. Anajua kilicho chini ya mkono wako, moyoni mwako. Na akujalie, ndilo ombi langu.

72 Mungu mpenzi, kwa kuwa tunashukuru kwa ajili ya jengo hili ambalo sisi, watoto Wako wanyenyekevu, tunaweza

kukusanyika pamoja hapa chini, na kuzungumza tu na kufanya ushirika, kuwa tu sisi wenyewe, tunapojisalimisha kwa Kristo, na kutamani kuwa zaidi kama Yeye. Sisi ni ndugu wahudumu tulioketi karibu, Bwana, watu walio na uwezo zaidi wa kusimama hapa kulileta Neno hili kuliko mimi, mtumishi Wako asiyestahili, bali kura imeniangukia. Na, Baba, ninaomba, leo, ya kwamba kama huenda nikasema jambo fulani ambalo halingekuwa ni kulingana na mapenzi ya Mungu, ya kwamba, kabla sijalisema, ungekifunga kinywa changu; kama ulivyovifanya vinywa vya simba, siku moja, hivi kwamba hawangemsumbua Danieli.

73 Baba, tunakuomba sasa kumkumbuka kila mmoja, kila mhudumu. Na uamsho huu unaoendelea hapa mjini, Bwana, huko chini kwa Assemblies of God, ninaomba, Mungu mpenzi, ya kwamba Wewe utatuma uamsho mkuu sana mle ndani hata mji huu wote utasukwasukwa na Nguvu za Mungu, kwamba baa hizi zote na watoto wanaotangatanga huku mtaani wataletwa kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, na kujazwa na wema Wake na Roho Wake. Tujalie, Baba wa Mbinguni.

74 Na tunaomba ya kwamba leo, kwamba kukiwako na mwanamume ama mwanamke, mvulana ama msichana, ambaye ameletwa kwenye mkutano huu asubuhi ya leo, hapa chini ambapo tumekingwa na theluji, ya kwamba Roho Mtakatifu mkuu ataitembelea mioyo yao na kunena nao, katika njia ya kisiri. Huenda baadhi yao ambao wamepotea, ambao wakati mmoja walikukaribisha Wewe, Bwana, lakini sasa wameondoka; warudishe, Bwana, asubuhi ya leo.

75 Na tunaliombea tawi hili, tunamwombea Ndugu Earl na mke wake, na kwa ajili ya wengine. Tujalie, Bwana.

76 Sasa tumegee Mkate wa Uzima, tunapozifungua kurasa za Neno, kwa sababu tunajua Biblia si ya kufasiriwa apendavyo mtu binafsi. Lakini, Mungu hatuhitaji sisi tulifasiri Neno Lake, Yeye Ndiye mfasiri Wake Mwenyewe. Yeye alisema siku moja, "Iwe nuru," na ikawa nuru. Alisema, "Bikira atachukua mimba," naye akachukua. "Na katika siku za mwisho nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili," haidhuru ulimwengu ulisema nini, Yeye aliimwaga. Hahitaji mfasiri yeyote. Yeye huyafasiri Maneno Yake Mwenyewe, kwa kuyafanya hai na kuyathibitisha kuwa hivyo. Ingia mioyoni mwetu, Bwana Yesu, na utufasirie, leo, mambo tunayohitaji. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

77 Sasa katika Biblia, kama mtafungua. Ninaamini sijapata kuwa na Ujumbe ambao nilijaribu kujiandaa kuuhubiri, ambapo kwanza sikulisoma Neno. Kwa kuwa, neno langu litashindwa, mimi ni mwanadamu. Lakini Neno Lake kamwe haliwezi kushindwa, Yeye ni Mungu. Kwa hiyo hebu na tufungue sasa kwa ajili ya fungu dogo tu, nasi tutatoka katika muda wa kama dakika thelathini, arobaini, Bwana akipenda.

78 Kwenye Ufunuo sasa, tunataka kufungua mlango wa 3 wa Ufunuo, kuanzia kifungu cha 14. Na tunataka kusoma sehemu yake tu, ni Ujumbe kwa Wakati wa Kanisa la Laodikia. Na ninaamini, nami—nadhani karibu watu wote waliojazwa na Roho na wasomi wa Biblia wanaamini, wangeweza kusema *amina* kwa hilo, ya kwamba tuko katika Wakati wa Kanisa la Laodikia, kwa maana huo ndio wakati wa mwisho. Usikilizeni Ujumbe wa hali ya kanisa kwenye wakati huu.

> *Na kwa malaika wa kanisa lililoko*. . .Laodikia *andika: Haya ndiyo anenayo yeye aliye Amina, Shahidi aliye mwaminifu na wa kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu.*
>
> *Nayajua matendo yako,*. . .*hu baridi wala moto; ingekuwa heri* kama *ungekuwa baridi au moto.*
>
> *Basi, kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, ninakutapika utoke katika kinywa changu.*
>
> *Kwa kuwa wasema, Mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu; wala hujui ya kuwa wewe ni mnyonge,*. . .*mwenye mashaka,*. . .*maskini,*. . .*kipofu, na uchi.*
>
> *Nakupa shauri, ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa*. . .*moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona.*
>
> *Wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidii, ukatubu.*
>
> *Tazama, nasimama mlangoni, nabisha: mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami.*
>
> *Yeye ashindaye, nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, kama mimi* nilivyoshinda *nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi.*
>
> *Yeye* aliye *na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.*

79 Bwana na abariki kusomwa kwa Neno hili. Sasa ninataka kuchukua, kwa dakika chache tu, somo dogo, linaloitwa, *Milango Ndani Ya Mlango*. *Milango Ndani Ya Mlango*. Sasa hili ni ninii sana. . .*Milango Ndani Ya Mlango*, ni maneno manne. *Milango Ndani Ya Mlango*.

80 Unaweza ukaniambia, "Ndugu, huenda ikawa hapa pana watu mia moja. Hapo, hivi hudhani kwamba kwa namna fulani hilo ni fungu dogo la maneno, wakati mbele yako unao watu mia moja?"

81 Vema, hilo, huenda hilo likawa ni kweli, fu—fungu la maneno ni dogo. Bali si ukubwa wa fungu la maneno, ambao—ambao unajalisha, ni kile lilicho. Ni—ni kile fungu hilo la maneno linachosema, hilo ndilo muhimu.

82 Kama vile, ninaamini ilikuwa huko Louisville, Kentucky, muda fulani uliopita, m—mvulana mmoja mdogo alikuwa darini, akipekua-pekua makasha ya zamani kwenye kijumba cha orofani, naye akapata stempu ya posta ya mtindo wa kale. Vema, jambo la kwanza mawazoni mwake, huenda akapata koni ya aiskrimu kwa hiyo. Kulikuwako na mkusanya huko chini mtaani, kwa hiyo akaenda mbio mtaani, upesi tu alivyoweza kukimbia. Na akasema, "Utanipa nini kwa stempu hii?"

83 Huyo mkusanya akaiangalia kwa makini, nayo kidogo ilikuwa imepauka. Akasema, "Nitakupa dola moja."

84 Jamani, hiyo iliuzika kwa urahisi. Angalikubali kuiuza kwa shillingi moja, na angefurahia jambo hilo, akanunue aiskrimu, bali iliuzwa kwa dola moja. Mkusanya huyo akaiuza kwa dola mia tano. Halafu baadaye, sijui kweli ilienda wapi, iliuzwa kwa mamia ya dola. Unaona, kipande hicho kidogo cha karatasi hakikuwa na thamani kubwa, ni kipande tu ambacho usingalikiokota sakafuni. Lakini, karatasi siyo iliyojalisha, ni kile kilicho kwenye karatasi hiyo, ndicho kinachojalisha.

85 Na hivyo ndivyo ilivyo katika kulisoma Neno la Mungu. Si karatasi tu, thamani ya karatasi hiyo, au ukubwa wa karatasi hiyo, ni kile kilichoandikwa kwenye karatasi hiyo. Nalo neno moja linatosha kuuokoa ulimwengu, kama likipokewa jinsi hiyo.

86 Wakati fulani uliopita kulikuwako. . . Nilisoma hadithi ya nanii wetu mkuu. . . Mmoja wa marais wakuu sana nafikiri taifa hili liliyepata kuwa naye alikuwa—alikuwa ni Lincoln. Sio kwa sababu alitoka Kentucky, bali ni kwa sababu alikuwa ni mtu mashuhuri. Hakupata elimu, bali hata hivyo alikuwa—alikuwa na kitu moyoni mwake, kusudi fulani.

87 Na—nampenda mtu mwenye ono. Ninawapenda watu walio na jambo fulani wanalopigania, sio tu kukaa vivi hivi, "Vema, chochote kijacho kitakuwa ni sawa." Loo, fanya hima ushike kazi! Wala Lincoln hakuiruhusu elimu yake imzuie; alikuwa na jambo fulani la kufanya. Nafikiri kila Mkristo anapaswa kuwa jinsi hiyo, ugundue kusudi lako na uende ukalitekeleze.

88 Kila memba wa tawi hili, sio tu, "Vema, tuna kiamshakinywa mara moja kwa mwezi," hilo silo, "ama mara moja kila Jumamosi." Kuwa na kusudi fulani maishani, jambo fulani utakalofanya. Hebu. Mungu amekuweka hapa; fanya jambo fulani kulihusu, kila mfuasi wa kila kanisa. Kuna uamsho mjini. Uamsho huo uko humo kwa kusudi fulani. Hebu na tupate kitu fulani kutoka kwake. Hebu na tufanye jambo fulani kuuhusu.

89 Bw. Lincoln. Kulikuwako na mtu ambaye. . . jamaa mdogo, a—alikuwa vitani, na—naye alikuwa—alikuwa ni mwoga,

kwanza. Na wakati wa kazi, a—a—aliondoka kazini; nao wakapata jambo fulani dhidi yake, ambapo alikuwa atapigwa risasi. Na, loo, yeye . . . lilikuwa ni jambo baya sana. Na jamaa mmoja kijana alimpenda sana, akamwendea Bw. Lincoln, akapate msamaha. Alikuwa ndiye rais wakati huo, Marekani hapa, na kwa hiyo akamwendea apate msamaha.

90 Ndipo akamwambia, wakati akitoka kwenye gari lake la farasi; na Bw. Lincoln, mtu halisi wa kusini, mrefu, mwenye mandevu, mwembamba sana. Naye akasema, "Bw. Lincoln, yupo mvulana atakayekufa, katika siku mbili tangu sasa, kupigwa risasi, kwa kuwa alitoroka wakati wa vita." Naye akasema, "Bw. Lincoln, mvulana huyo si mvulana mbaya. Lakini bunduki hizo zote za mirao zikifyatua risasi, na—na watu wakifa, yeye alikuwa na wasiwasi. Naye alifadhaika sana, hata, aliitupa mikono yake juu na akaanza kupiga makelele." Akakimbia pale, akasema, "Nimemjua mvulana huyo." Kasema, "Bw. Lincoln, ni jina lako tu kwenye karatasi hii linaloweza kumwokoa. Je! utamwokoa?

91 Bila shaka, muungwana huyu Mkristo, upesi alitia sahihi karatasi hiyo, "Amesamehewa, *Fulani-wa-fulani*." Akaandika jina lake, "Abraham Lincoln, Rais wa Marekani."

92 Huyo mjumbe akarudi upesi alivyoweza. Akakimbilia kwenye seli, akasema, "Uko huru! Uko huru! Hii hapa ya Bw. Lincoln, sahihi ya Bw. Lincoln. Uko huru!"

93 Akasema, "Kwa nini unakuja kunidhihaki, ukijua ya kwamba nafa kesho?" Akasema, "Kiondolee hicho mbali na hapa, unanidhihaki tu." Wala asingekipokea. Akasema, "La, si—sikitaki." Kasema, "Unafanya tu . . . " Kasema, "Kama hiyo ilikuwa ni Ra—Rais," kasema, "ingekuwa na ne—nembo, na ingekuwa kwenye karatasi yake rasmi."

Akasema, "Lakini ni sahihi yake!"

94 Akasema, "Nitajuaje sahihi yake?" Akasema, "Unanidhihaki tu, unajaribu kunifanya nijisikie vizuri." Ndipo akaanza tu kupaza sauti, akampa kisogo. Mvulana huyo alipigwa risasi kesho yake asubuhi.

95 Ndipo baada ya mvulana huyo kufa, na jina la Rais kwenye karatasi hii, kwamba alikuwa amesamehewa, basi vipi? Nao wakalijadili kwenye mahakama ya shirikisho. Nao huu hapa uamuzi wa mahakama zetu za shirikisho, ambayo ndiyo mkataa wa mahakama zetu zote. Wanachosema wakati mwingine, hatupendezwi na uamuzi wao, bali hatuna budi kuutii kwa vyovyote vile, unaona, kwa maana hilo ndilo neno la mwisho. Huo ndio mkataa. Sasa, ilitoa uamuzi huu, "Msamaha si msamaha isipokuwa upokelewe kama msamaha."

96 Na hivyo ndivyo lilivyo Neno la Mungu. Ni msamaha kama likipokelewa kama msamaha. Na ni Neno la Mungu, ni nguvu za Mungu, kwa wale watakaoliamini na kulikubali.

97 Haidhuru, unaliangalia, na kusema, "Loo, hilo limevurugwa kabisa, kumekuwako na tafsiri milioni moja, na yote hayo." Huenda ikawa hivyo kwa mtu fulani.

98 Lakini, kwangu mimi, lingali ni Neno la Mungu, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Yeye anawajibika kudumu kwenye hilo Neno.

99 Sasa Yeye hana budi kulihukumu kanisa, siku moja. Na kama akilihukumu kwa kanisa Katoliki, ambalo wao wanasema atalihukumu kwalo, basi ni lipi kati ya makanisa ya Katoliki atakalolihukumu kwalo? Yanatofautiana moja na lingine. Kama akiuhukumu kwa la Methodisti, ninyi Wabaptisti mmepotea. Kama akilihukumu kwa la Kipentekoste, ninyi wengine mmekwisha.

100 Lakini hatauhukumu kwa kanisa. Biblia ilisema, "Yeye atauhukumu ulimwengu kwa Yesu Kristo, na Kristo ni Neno." Kwa hiyo unaona hatuna udhuru, ni Neno la Mungu, ambalo atatuhukumu kwalo; na haidhuru ni dogo jinsi gani, Neno moja ni muhimu kwa Hili, Ufunuo 22:18 ulisema.

101 Kwanza, nitaanzia katika Mwanzo. Mungu aliipa jamii ya binadamu Neno Lake, wajikinge na mauti, dhambi, na huzuni, ama maafa yoyote. Mnyororo, wa Maneno Yake. "Usiuguse mti fulani huu, kwa kuwa, siku utakayoula, siku hiyo utakufa." Na mnyororo uko katika hali yake iliyo nzuri sana kwenye kiungo chake kilicho dhaifu sana. Na nafsi zetu zinavutwa juu ya kuzimu, zikiushikilia mnyororo huu; ukikata kimoja, hilo tu ndilo linalokubidi kufanya. Hawa kamwe hakuvunja sentensi, alivunja Neno moja, kupitia Shetani. Huo ulikuwa ni mwanzoni mwa Kitabu.

102 Katikati ya Kitabu akaja Yesu, na akasema, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno." Sio sehemu yake, moja tu hapa na pale, lakini, "Kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu."

103 Wakati alipokuwa amekufa, akafufuka, na akaenda Mbinguni, kisha akarudi na kumpa Yohana . . . ambalo alisema pale baada ya kufufuka Kwake. Alisema, "Vipi kama . . ." Kasema, "Itakuwaje kwa mtu *huyu*?"

104 Yesu alisema, "Imekupasaje kama akiendelea hata nijapo?" Akijua sio uhai wake hasa ungeendelea, bali huduma yake ingeendelea. Naye akamtwaa juu, katika mlango wa 4 wa Ufunuo, na kumwonyesha mambo yote yatakayokuja, ambayo kwayo tunaishi, hata kufikia kwenye fungu hili leo.

105 Na halafu katika mlango wa 22, ule mlango wa mwisho, kifungu cha 18, Yeye alisema, "Mtu yeyote atakayeondoa Neno moja kutoka katika Kitabu hiki, au kuongeza neno moja Kwake, ataondolewa sehemu yake kutoka katika Kitabu cha Uzima." Unaona? Kwa hiyo tunaamini ya kwamba mtu huishi kwa kila Neno la Mungu. Ninaamini hilo na ninajua ni kweli. Liwe ni

dogo jinsi gani, haijalishi. Inachukua tu neno moja, kufanya jambo hilo.

106 Nikiwazia lilivyo jambo dogo na nyonge, nikiona kuwa wengi wa marafiki zangu wa Kanada wanaoketi hapa. Ninakumbuka nilikuwa Kanada wakati Mfalme George . . . Yule niliyekuwa na majaliwa ya kwenda na kumwombea, wakati alipoponywa, akiwa na ugonjwa huo wa kukacha kwa seli; alikuwa akiumwa siku hiyo, kutokana na mkachuko wa seli, naye pia alikuwa anaumwa na tumbo, vidonda vya tumbo, kama vile wengi wenu Wakanada mjuavyo, na Wamarekani, pia. Lakini tukimwona akipitia pale, ameketi kwenye hilo gari la farasi, yeye—yeye alikuwa ni mfalme. Alitenda kama mfalme. Malkia wake mrembo ameketi karibu naye, amevaa nguo yake ya bluu, na wakati akishuka kuja barabarani.

107 Na mimi, pamoja na rafiki yangu, tulikuwa tumesimama pamoja. Na wakati gari lile lilipopitia hapo, yeye aligeuza tu kichwa chake akaanza kulia. Nikauweka mkono wangu juu ya bega lake, na nikasema, "Kuna shida gani?"

108 Akasema, "Ndugu Branham, yule pale mfalme wangu na malkia wake wanaenda." Vema, ni—ningeweza kufurahia jambo hilo.

109 Kwa hiyo nikawazia, "Kama Mkanada, chini ya kiongozi wa serikali, sio kiongozi wa serikali, bali pia ni kiongozi wa serikali, ya Uingereza, na mfalme akipitia pale, lingemfanya Mkanada kulia, na kukigeuza kichwa chake na kulia, itakuwaje tutakapomwona Mfalme wetu?" Na kuwazia jambo hilo, sehemu yetu itakuwa ni Malkia.

110 Ndipo watoto wote walikuwa wametolewa shuleni, watoto wadogo, walipewa bendera ndogo, za Uingereza. Bendera ya Kanada inaitwa kitu kingine. Ndugu Fred, bendera ya Kanada inaitwaje? [Ndugu Fred Sothmann anasema, "Union Jack."—Mh.] Union Jack. Lakini waliwapa bendera ndogo ya Uingereza, kupeperusha. Na wakati mfalme huyo alipopitia pale, watoto wote wadogo walisimama, wakizipeperusha ninii yao—bendera yao ndogo, na kumshangilia mfalme. Na—na kulikuwako na bendi zikicheza, *Mungu Mwokoe Mfalme*, wakati akipita katika maandamano mtaani.

111 Loo, laiti ungaliweza tu kupata ninii . . . Ungepata fununu ya jinsi itakavyokuwa kwenye ule ufufuo kule!

112 Na wakati walipoagizwa, hao watoto wadogo, kurudi shuleni mara tu gwa—gwaride lilipokwisha. Na, watoto hao wadogo wakirudi, shule moja ilimkosa msichana mmoja mdogo. Nao wakaenda kila mahali, kumtafuta maskini jamaa huyo mdogo, huku na huku mitaani. Basi, hatimaye, nyuma ya nguzo ya simu, kilisimama kijitoto kidogo, kidogo sana, kisichana kilichodumaa, kikilia tu kwa moyo wake wote.

113 Vema, mwalimu akamchukua na . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] "Ni nini? Je! hukumwona mfalme?"

Akasema, "Ndiyo, nilimwona mfalme."

Akasema, "Je!—je! hukuipeperusha bendera yako?"

Akasema, "Ndiyo, ni—niliipeperusha bendera yangu."

Akasema, "Vema, basi, kwa nini unalia?"

114 Akasema, "Unaona, mwalimu, mimi ni mdogo sana, hao wengine walikuwa wamesimama mbele yangu, walikuwa ni wakubwa zaidi. Nami niliipeperusha bendera yangu, bali hakuiona." Naye alisumbuliwa na jambo hilo. Vema, hilo linawezekana kwamba Mfalme George hakumwona jamaa huyo mdogo, kwa kimo. Huenda hakuona moyo wake wa uzalendo, na jinsi alivyojisikia juu yake. Alikuwa ni mfupi sana.

115 Bali sivyo ilivyo na Mfalme wetu! Loo, jambo dogo sana tunalofanya, Yeye huliona. Naye anajua mambo yenyewe na mawazo yaliyo mioyoni mwetu, lolote tufanyalo, hata liwe ni dogo jinsi gani. Nasi tunamtumikiaje? Tunapotumikiana mmoja kwa mwingine. Kama siwapendi, ninawezaje kumpenda Yeye? Unaona? "Kadiri mlivyowatendea hawa wadogo Wangu, mmenitendea Mimi." Mnaona?

116 Ni—ni mambo madogo tunayoyaacha bila kuyashughulikia, wakati mwingine, ambayo hukata mnyororo wote, unaona, na kutuweka huru, nia za kimadhehebu tu, na kusahau mambo haya madogo ambayo kweli ndiyo mambo yaliyo mu—muhimu. Kila kitu, kila Neno la Mungu, ni muhimu. Hakuna hata moja linaloweza kuachwa. Hatuna budi kuchukua kila Neno Lake, jinsi tu lilivyoandikwa.

117 "Ninasimama mlangoni," alisema Yesu, katika Wakati huu wa Laodikia, "na kubisha." Je! mliona, ule wakati pekee wa kanisa aliowekwa nje ya kanisa Lake? Nyakati zingine zote za kanisa, Yeye alikuwa ndani ya kanisa. Kwa Wamethodisti, na Walutheri, na kadhalika, Yeye alikuwa ndani, kanisa. Lakini hapa Yeye yuko nje, kanuni zetu za Imani na kadhalika zilikuwa zimemtoa nje ya kanisa. Lakini Yeye anasimama huko nje, angali anabisha, "Yeye atakayesikia na kuufungua mlango, nitaingia pamoja naye, kula pamoja nao, na kumpa uponyaji wa macho yake, na—na nguo, na kumpa utajiri wa Mbinguni; yeye atakayenisikia nikibisha."

118 Nilidhani ningekumbuka jina la yule mwanasanaa aliyeichora ile picha, aliyeitia rangi picha, hasa, ya kuwa mlangoni. Wakati yeye . . . Mwajua, picha zote maarufu kwanza hazina budi kupitia kanuni, ama, ukumbi wa wakosoaji, kabla haijatundikwa kwenye Ukumbi wa Umaarufu. Hiyo picha awali iliyotiwa rangi sasa ingegharimu mamilioni ya dola.

119 Lakini, mnaona, ni kama vile Kanisa, halina budi kupitia kwenye ukumbi wa wakosoaji. Tunaupitia. Utaitwa "mtakatifu

anayejifingirisha," utaitwa kila kitu. Lakini kama tu ungeweza kupashikilia mahali pako katika Kristo, basi siku moja Yeye atatupeleka kwenye Ukumbi wa Umaarufu. Lakini kwanza hatuna budi kustahimili ukosoaji. Hapo ndipo udogo wetu unaposimama, hapo ndipo unapoonyesha. "Yeye asiyeweza kustahimili marudio ni mwana haramu, wala si mwana wa Mungu." Haidhuru amejiunga na kanisa jinsi gani, na lolote alilofanya, yeye angali, kama hawezi kustahimili marudio, yeye ni wa haramu, wala si mwana halisi wa Mungu. Lakini mwana halisi, wa kweli wa Mungu hajali yale ulimwengu usemayo, kitu kingine chochote huja baadaye. Nia yake iko kwa Kristo, na hilo latosha. Naam. Lolote Kristo asemalo lifanywe, atalifanya. Popote Mwana-Kondoo aendako, wako pamoja naye, popote pale. Halafu mnaona kuonekana Kwake, Uwepo Wake, na kile afanyacho. Yeye daima yupo pamoja na watu Wake, Bibi-arusi Wake. Yeye anamposa. Siku moja kutakuwako na Chakula cha Jioni cha Arusi.

120 Na mwanasanaa huyu, lakini, wakati ilipopitia kwa wakosoaji, kundi la wakosoaji lilimzunguka mwanasanaa huyu. Siwezi kulikumbuka jina lake. Ninajaribu kumkumbuka Michelangelo, ila alikuwa ndiye aliyeichonga sanamu ya Musa. Lakini siwezi kukumbuka jina lake. Lakini, hata hivyo, alisema, "Picha yako ni nzuri sana," kasema, "sina neno ningaliweza kusema dhidi ya picha hiyo." Akasema, "Kwa sababu, anashika kandili mkononi mwake, inaonyesha ya kwamba Yeye anakuja, pia, wakati wenye giza totoro usiku." Akasema, "Na halafu yuko mlangoni, pamoja na kichwa Chake, sikio Lake, kwa hiyo hataninii. . .ahakikishe hatakosa mwito wa sauti iliyo ndogo sana. Ameelekeza sikio Lake mlangoni, Naye anabisha mlangoni." Akasema, "Lakini, unajua, bwana, kuna kitu kimoja ulichosahau kwenye picha yako."

121 Naye mwanasanaa huyo, ilimchukua muda wa maisha yake kuichora, akasema, "Ni kitu gani hicho ambacho nimesahau, bwana?"

122 Akasema, "Haidhuru alibisha kiasi gani, unaona, ulisahau kuuwekea komeo. Hakuna komeo mlangoni." Kama utauangalia huo mlango, hauna komeo.

123 "Loo," kasema mwanasanaa huyo, "niliitia rangi hivyo. Unaona, bwana," akasema, "komeo liko upande wa ndani. Wewe ndiwe unayeufungua mlango. Unaufungua mlango."

124 Loo, ni kwa nini mtu anaubisha mlango wa mtu? Anataka kuingia. Anataka aingie ndani. Labda ana jambo analotaka kukwambia ama kuzungumza na wewe. Ana ujumbe kwa ajili yako. Na hiyo ndiyo sababu watu hubisha mlango wa mmoja kwa mwenziwe. Wanayo sababu ya kufanya hivyo. Hilo haliwezi kutukia bila ya sababu fulani. Usingeweza kwenda kwenye nyumba ya mtu fulani pasipokuwa na sababu ya kufanya hivyo;

kama hakuna kitu kingine, kutembelea, kumpelekea ujumbe, ama kitu fulani. Kuna sababu ya mtu kwenda kubisha mlango wa mtu mwingine.

125 Popote palipo na swali, hapana budi pawe na jibu. Kusingeweza kuwako na swali bila jibu. Kwa hiyo hilo ndilo tunaloangalia katika Biblia, maswali haya ya siku hizi, Biblia inalo jibu. Naye Kristo Ndiye Jibu hilo.

126 Sasa, watu wengi mashuhuri wamebisha milango, kote katika wakati wa maisha, na wengi walibisha katika nyakati zilizopita; na labda, nyakati zikiendelea, kutakuwako na wengi zaidi, watu mashuhuri.

127 Sasa, jambo la kwanza, labda, kama mtu alibisha mlangoni pako, kama ungaliweza, ungenyemelea na kufungua pazia, uone ni nani aliye hapo.

128 Kama una shughuli nyingi, kama tunavyodai tunazo siku hizi, "Shughuli nyingi mno hata hatuwezi kwenda kanisani; shughuli nyingi mno hatuwezi kufanya jambo *hili*. Na, mwajua, kanisa langu haliamini upuuzi wa namna hiyo." Na, mnaona, kidogo tuko nje, wakati mwingine, ya Neno.

129 Lakini ukivuta pazia, basi unataka kuona ni nani anayesimama pale. Na kama ni mtu mashuhuri, upesi unakimbia mlangoni.

130 Sasa hebu na turudi nyuma kidogo tu, na tuwachukue watu wachache ambao wamebisha. Hebu na turudi nyuma na tuwazie juu ya Farao kule Misri, miaka mia kadhaa iliyopita. Vipi kama—kama Farao, mfalme wa Misri, alishuka kuja kwenye nyumba ya mkulima mdogo? Na mkulima huyu mdogo alikuwa kidogo hakubaliani na Farao, wala hakuamini sera zake, naye alitofautiana naye. Na—na, lakini huyu hapa Farao amesimama, amesimama mlangoni mwa mwa—mwashi ama mkandikaji wa matope, kama vile tungaliwaita, huko Misri. Naye anafungua pazia lake, na huyo hapo amesimama Farao mkuu mlangoni. Naye anabisha; tabasamu usoni mwake. [Ndugu Branham anagonga-gonga kitu fulani—Mh.] Mbona, mkulima huyo mdogo angeufungua mlango, na kusema, "Karibu ndani, ewe Farao mkuu, naomba mtumishi wako duni apate rehema machoni pako. Kama kuna kitu fulani chochote ndani ya nyumba yangu, mimi ni kama mtumwa kwako, Farao. Umeniheshimu kuliko ndugu zangu. Umekuja nyumbani kwangu, wakati mimi nikiwa maskini. Wewe huwatembelea tu wafalme na—na malodi, na watu mashuhuri. Nami ni mtu asiye na maana. Lakini wewe—wewe umenitembelea, umeniheshimu mimi, Farao. Ni kitu gani mtumishi wako duni angeweza kufanya?" Haidhuru Farao angeomba nini, hata uhai wake, yeye angempa. Hakika. Ni heshima.

131 Ama, tuseme kwa mfano, marehemu Adolf Hitler, wakati alipokuwa Mtawala wa Ujerumani. Vipi kama angalishuka

kwenda nyumbani kwa askari mmoja? Na kundi hilo la maskini askari wa Kinazi wote wamepiga kambi huko, na, muda si muda wajua, mbona, mtu fulani alibisha mlangoni. Na maskini askari huyo akasema, "A-ha, ninajisikia vibaya asubuhi ya leo! Mke wangu, waambie waende zao."

132 Naye angechoropoka aende mlangoni, na kuvuta pazia. Akasema, "Mume wangu! Mume wangu, inuka haraka, upesi!"

"Kuna nini? Ni nani anayesimama hapo?"

"Hitler, Mtawala wa Ujerumani!" Loo, jamani!

133 Maskini askari huyo akaruka akatoka, akavaa nguo zake, upesi, na akasimama mguu sawa. Akaenda mlangoni, akaufungua mlango, kisha akaufungua mlango, na kusema, "Salamu Hitler!" Unaona, yeye alikuwa ni mtu mkuu, siku zake huko Ujerumani. "Nifanye kitu gani?"

134 Kama angelisema, "Nenda ukaruke kutoka kwenye lile genge pale," angalifanya hivyo. Kwa nini? Hakuna mwingine, hakuna mtu mwingine aliye muhimu katika Ujerumani, katika siku za Wanazi, kuliko Adolf Hitler alivyokuwa. Yeye alikuwa ni mtu mashuhuri. Na yeye . . . Na, ni heshima jinsi gani, wakati yeye huwatembelea tu majemadari na watu mashuhuri, bali huyu hapa mlangoni pa maskini mtumishi! Loo, bila shaka ingekuwa ni heshima kubwa kwake.

135 Vema, sasa, ni vipi kuhusu Flagstaff? Tutalileta karibu na nyumbani. Vipi kama alasiri ya leo, kwamba—kwamba Rais wetu, Bw. Johnson, L. B. Johnson, vipi kama angetoka kwenye ndege, hapa nje mahali fulani? Na sasa sisi sote tuko kwenye tabaka moja la watu. Sisi sote ni maskini. Labda mmoja ana kazi bora zaidi kidogo, labda nyumba nzuri zaidi kidogo, lakini, hata hivyo, sisi sote ni wanadamu tu. Lakini vipi kama akishuka kuja nyumbani kwako hapa chini, labda mmoja wetu aliye duni kuliko wote, na akabisha mlangoni; nawe ukaenda mlangoni, na huyo hapo Rais L. B. Johnson amesimama? Mbona, ingekuwa ni heshima kubwa. Huenda usikubaliane naye, katika siasa. Bali ungekuwa ni mtu aliyeheshimika, kuwa na Rais wa Marekani amesimama mlangoni pako. Wewe ni nani ama mimi ni nani? Na huyo hapo Lyndon Johnson amesimama mlangoni pako! Ingawa huenda ukawa u Msoshalisti ama Mwanachama wa Jamhuri, ama unatofautiana naye kwa maili milioni moja, bali hata hivyo bado ingekuwa ni heshima.

136 Unajua nini? Kwa kuwa ulipewa heshima hii, mbona, televisheni ingeitupa kwenye skrini usiku wa leo. Hakika. Magazeti ya kesho mchana yangekuwa na vichwa vya habari ndani yake, huku katika gazeti la Flagstaff, kwamba, "*John Doe*. Rais wa Marekani aliruka kwa ndege mpaka Flagstaff jana, bila kutarajiwa, naye akashuka tu akaenda, bila hata mwaliko, na kubisha" mlangoni pako. Mnyenyekevu! Rais huyo angepata jina la kuwa mtu mnyenyekevu, ingawa ni mkuu kama alivyo, kuja

mlangoni pangu ama mlangoni pako; sisi si kitu, kisha anashuka anakuja kuongea nasi.

137 Mbona, ungetembea mtaani, na kusema, "Naam, mimi ndimi mwenyewe. Rais alinitembelea."

138 "Simama kimya, hebu nipige ninii yako—nipige picha yako. Niangalie moja kwa moja. Sasa unaonekanaje wakati unapoondoka?" Ungekuwa ni mtu mashuhuri. Hakika.

139 Vipi kama malkia wa Uingereza angekuja, ingawa wewe huko chini ya utawala wake? Lakini ingekuwa ni heshima kwa baadhi yenu wanawake kumkaribisha malkia wa Uingereza, ingawa hamko chini ya utawala wake. Lakini, hata hivyo yeye ni mtu mashuhuri, yeye ndiye malkia mkuu kuliko malkia wote ulimwenguni, wakati huu. Hakika, ndivyo alivyo, hiyo ni kunena kisiasa. Lakini kama angalikuomba kipambo kidogo ukutani mwako, ambacho ulikithamini sana, ungalimpa. Ingekuwa ni heshima kwako kufanya jambo hilo. Hakika, yeye ni malkia wa Uingereza.

140 Nawe ungeheshimiwa, na Rais. Na kila mtu angezungumza juu ya unyenyekevu wa malkia wa Uingereza, akiruka kwa ndege kwenda kumwona mwanamke fulani huku Flagstaff, maskini mtu hohe hahe. Na magazeti yangeandika hilo, na habari zingelitangaza.

141 Lakini, unajua, Mtu aliye muhimu kuliko wote wa wakati wote, Yesu Kristo, anaubisha mlango wetu. Naye anakataliwa, mkuu kuliko wafalme wote na watawala waliopata kuwapo. Hiyo ni kweli. Nawe huenda ukamkubali na utoke uende ukaseme jambo fulani kulihusu, ulimwengu wa nje ungekucheka waziwazi. Hakuna habari itakayoninii . . .

142 Ni nani angeweza kuja nyumbani mwako, aliye mkuu zaidi ya Yesu Kristo? Ni nani angaliweza kuubisha mlango wako, aliye mkuu kuliko Yesu Kristo? Ni nani angaliweza kufanya hivyo? Mwana wa Mungu, ni nani angeweza kubisha nyumbani mwako, ambaye angekuwa ni muhimu zaidi? Na hata hivyo Yeye hubisha, siku baada ya siku. Na kama hata ukimkubali, unaitwa mlokole. Kwa hiyo, unaona jinsi ulimwengu unavyowajua walio wake? Hiyo ni kweli. Lakini sasa Yeye asingekuja isipokuwa alikuwa na sababu ya kuja.

143 Na je! unafikiri unyenyekevu wa Rais Johnson, ama malkia wa Uingereza, ama mtu mwingine yeyote aliye mkuu, jinsi ambavyo ungeonyeshwa, wa unyenyekevu wa mtu huyo mkuu jinsi hiyo kubisha mlangoni pako!

144 Vipi kuhusu unyenyekevu wa Mwana wa Mungu? Sisi ni akina nani ila wenye dhambi, wachafu, "waliozaliwa katika dhambi, wakaumbika katika uovu, wakaja ulimwenguni wakisema uongo?" Na halafu Mwana wa Mungu atakuja na kubisha mlangoni petu.

145 Sasa, malkia wa Uingereza huenda akakuomba fadhili. Huenda akachukua kitu fulani kutoka kwako. Vivyo hivyo na Rais, huenda akakuomba ufanye jambo fulani usilotaka kufanya. Huenda akakuomba umpe hazina ambazo hukutaka kutoa, na ambazo hazingemaanisha kitu, kwake kabisa.

146 Lakini Yesu anakuletea kitu fulani anapobisha. Analeta msamaha. Usiukatae. Kwa kuwa, kama vile kesi ilifanyiwa huku kwenye mahakama zetu hapa, ndivyo itakavyokuwa katika Ufalme wa Mbinguni. Kama Yeye alibisha na kuleta msamaha, nawe ukaukataa, kisha ufe katika dhambi zako, utaangamia; ingawa ulikuwa na heshima ya kuketi kwenye mkutano kama huu, ingawa ulikuwa na heshima ya kuhudhuria uamsho, ama kanisa lako, na ukamsikia mchungaji wako akiuhubiri ujumbe wa Injili. Nawe ulikuwa na wasikilizaji, useme, "Naam, nilikuwapo pale." Pengine, wewe, ni vigumu kusema yote ungaliweza kusema. "Nilisikia uimbaji. Niliufurahia. Nilisikia shuhuda. Zilikuwa ni za kweli." Bali uliukataa.

147 Vipi kama ningalikuwa kijana mwanamume na nikampata msichana; alikuwa ni mrembo, alikuwa ni Mkristo? Angefaa kuwa . . . Alikuwa na kila sif- . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Huwezi kupata kosa lolote Kwake, bali inakubidi kuweka kando mapokeo ya wanadamu. Unasema, "Loo, ninaamini Hilo ni kweli. Ninaona, ninaninii . . . " Lakini inakubidi kulikubali. Wewe . . . Ndipo mwanamke huyo anakuwa ni sehemu yangu. Ndipo unakuwa sehemu ya Neno, ambalo ni Bibi-arusi. Kama Yeye ni Neno, Bibi-arusi atakuwa ni Bibi-arusi-Neno. Unaona, hakika atakuwa! Unaona, huna budi kulikubali. Ungeninii . . . Ungeweza kusema utakalo, ungeweza kujivunia Rais; lakini kwa kawaida wakati zamu ya Yesu ikija mlangoni petu, sisi tunamkataa tu. Unaona, hatutaki uhusiano wowote na Yeye. Tunasema, "Vema, siku nyingine."

148 Vipi kama ulibisha mlangoni pa mtu fulani? Sasa hebu kidogo na tuigeuze picha hiyo moja kwa moja kwa dakika moja. Vipi kama uliienda ukabisha kwenye mlango wa mtu fulani, nawe ulikuwa na kitu fulani kwa ajili yao? Na, hata hivyo, wao walikuwa kwako kidogo kama vile ungalikuwa kwa Mungu; vema, kama ukifanya hivyo, mbona, vema, bali huna masharti yoyote. Kwa hiyo ulipobisha mlangoni pa mtu fulani, nao wakachungulia dirishani, na kufunga pazia; ama au wanakuja mlangoni, na kusema, "Wakati mwingine!"

"Vema, ningetaka . . . "

149 "Sina wakati asubuhi ya leo!" Unajua ungefanya nini? Huenda ni jambo lile lile ningalifanya, na hao wengine, usingerudi huko tena.

150 Lakini si Yesu. "Ninasimama, na kubisha," anaendelea kubisha. [Ndugu Branham anaendelea kugonga kitu fulani—Mh.] Unaona? "Yeye atafutatafutaye," sio atafutaye.

"Atafutatafutaye! Yeye agongagongaye!" Gonga, gonga ni jambo linaloendelea, gongagonga! Unaona, "Yeye atafutatafutaye, yeye agongagongaye, utaninii . . . " Sio tu . . .

151 Kama ule mfano wa yule hakimu dhalimu. Yule mwanamke alienda na akataka jilipiza kisasi, kulipiza kisasi, bali asingeweza. Yeye . . . Sikuzote aliendelea kubisha na kusihi. Naye akasema . . . "Ili tu kumwondoa, nitampa haki na adui yake."

152 Ni zaidi sana vipi Baba wa Mbinguni! Unaona, inapaswa iwe ni sisi tunaobisha mlangoni Pake. Ilipaswa iwe ni Adamu akikimbia-kimbia huku na huku bustanini, akisema kwa sauti kuu, "Baba! Baba, Uko wapi?" Lakini badala yake, badala ya hilo, Mungu ndiye aliyekuwa akikimbia-kimbia huku na huku bustanini, "Mwanangu! Mwanangu, uko wapi?" Unaona, hiyo inaonyesha tu kile tulicho sisi. Daima tunajificha, badala ya kujitokeza moja kwa moja na kukiri jambo hilo. Tunajaribu kukimbia, kujificha nyuma ya kitu fulani. Hiyo ni tabia tu ya mwanadamu, tunayo namna hiyo. Naam, bwana.

153 Ungewapa watu hawa kilicho kizuri kabisa ulichokuwa nacho, kila kitu. Bali usingeninii, u—u—usingemkubali Yesu. Simaanishi wewe, bali ninamaanisha watu waliopo hapa.

154 Ama labda huenda ungesema jambo hili, unaweza ukasema, "Mhubiri, nilifanya tu jambo hilo. Ni—niliufungua moyo wangu nikamwacha Yesu aingie. Nilifanya hivyo miaka kumi iliyopita. Nilifanya jambo hilo miaka ishirini iliyopita." Vema, hilo huenda ikawa ni kweli kabisa, lakini je! hilo ndilo tu umefanya? Unaona?

155 Ninataka kukuuliza sasa. Kama ungemwalika mtu yeyote nyumbani mwako, na halafu unapoingia mlangoni . . . Mtu fulani alikukaribisha ndani, hasa, akasema, "Karibu ndani."

156 "Naam, nina kusudi, nitatoka nje ya mji na nitaheshimiwa, unaona." Hivyo ndiyvo watu wengi wanavyomkubali Kristo. "Nitaninii . . . Mimi—mimi ni mfuasi wa kanisa. Mimi ni mshiriki wa mahali *Fulani* pakubwa hapa chini, ambapo Dk. Ph. LL. anashiriki, unajua. Nalo ndilo kanisa lililo kubwa kuliko yote. Meya huhudhuria huko, na kila kitu, unajua. Mimi—mimi ni mfuasi wa kanisa hilo." Wanamwacha aingie, umbali huo tu. "Naam, nitamkubali Yeye," unaona, kwa ajili ya faida ya kibinafsi.

157 Lakini vipi basi wakati Yesu anapoingia moyoni? Watu wengi humkubali kwa kuwa hawataki kwenda jehanamu. Lakini Yesu anapoingia moyoni mwako, Yeye anataka kuwa Bwana. Sio tu Mwokozi; bali Bwana, pia. *Bwana* ni "utawala." Yeye huingia ndani ili—ili kuchukua mamlaka.

Sasa unasema, "Hiyo ni kweli, Ndugu Branham?" Hakika.

158 Vipi kama—kama nilikualika nyumbani kwangu, nawe ukaingia mlangoni? Nawe ukabisha mlangoni, nami nikaangalia nje, nikasema, "Naam, karibu ndani. Kama unaweza kunisaidia, vema, fanya hivyo. Lakini sasa, unapoingia sasa, sitaki uingilie mambo ya nyumba yangu. Wewe simama tu papo hapo mlangoni!"

159 Kumbukeni, somo letu ni "milango" ndani ya mlango. Sasa, ndani ya moyo wa mwanadamu kuna milango mingi midogo, na hiyo milango midogo hufunika mambo mengi sana. Kumkaribisha tu ndani, hilo halitoshi, wakati Yeye anapoingia.

160 Ninapoingia nyumbani mwako, kama ukinikaribisha mlangoni, mbona, kama ungesema, "Karibu ndani, Ndugu Branham. Nina furaha sana kukuona!"

161 Ningesema, "Vema, ni majaliwa kwangu kuja nyumbani kwako!"

162 "Loo, hivi huwezi kuja na kuketi chini? Ndugu Branham, tembea katika nyumba yetu, jisikie nyumbani!" Loo, jamani!

163 Ningeenda kwenye friji, nitoe moja ya sambusa hizo kubwa sana, kama *hivi*, nivue viatu vyangu, na kuingia kwenye chumba cha kulala na kujilaza. Nami ningekuwa na—na yubile kwelikweli ya mlo, unaona. Kwa nini? Kwa maana nilijisikia kukaribishwa. Ulinikaribisha. Kwa hiyo ningefurahia jambo hilo kama ulinikaribisha.

164 Lakini kama nilienda nyumbani kwako, nawe ukaniambia, "Wewe simama hapo mlangoni, sasa, usianze kuingilia mambo huku!" Nisingejisikia kukaribishwa vizuri sana. Nawe je? La, unaona, usingejisikia kukaribishwa. Mtu fulani alikukaribisha uingie, na kusema, "Sasa ngoja! Naam, karibu ndani, bali usimame papo hapo!"

165 Sasa, upo mlango mdogo unapoingia kwenye moyo wa binadamu. Tutazungumzia tu baadhi ya hiyo, unaona. Hatuna wakati wa kupitia milango hii yote, maana kuna mingi sana. Unaona? Lakini, tuseme, kwa dakika kumi zijazo, hebu tuzungumzie baadhi yake, milango mitatu.

166 Sasa, upande wa kuume wa moyo wa mwanadamu, unapoingia mlangoni, upo mlango mdogo upande wa kuume, na huo unaitwa, mle ndani, mlango wa majivuno. Loo, jamani! "Usithubutu kuingia kwenye mlango huo!" Hawamtaki Bwana humo ndani, kwenye mlango huo, huo ni majivuno. "Mimi nina damu ya bluu. Ninashughulika! Loo, naam, sasa angalia, nakwambia, mimi—mimi . . ." Unaona, ni majivuno. "Usiingilie mambo mle!" Sasa, Yeye hawezi kujisikia amekaribishwa mradi tu unaendelea kuufunga mlango huo wa majivuno.

167 Yeye hana budi kukuaibisha. Unaona, hiyo ndiyo sababu ya kuja Kwake. "Unataka kuniambia ya kwamba inanipasa kushuka kwenda kule na—na kutenda kama hao wengine?"

Vema, si lazima uende, hilo ni jambo moja la hakika. "Vema, nitakuambia, unafikiri ningefanya nini wakati nilipoenda kwenye halmashauri ya biashara tena? Ningefanya nini kama nilikutana na mwajiri wa—wangu kesho? Na hilo, ingenilazimu kumpata huyo Roho juu yangu, nami ningeruka juu kule, katikati ya kazi yangu, na nianze kunena kwa lugha, loo, hilo lingeniabisha. La, usikaribie hapo!"

168 Unaona, haya basi, unaona. Naam, utamruhusu Yesu aingie, utajiunga na kanisa na kuandika jina lako, umkubali Yesu kama Mwokozi wako; bali vipi kuhusu kuwa Bwana wako, wakati akiwa na mamlaka kamili? Wakati anapokuwa ni Bwana, yeye ana yote, u mali Yake; wewe, wewe umejitolea kabisa Kwake sasa.

169 Lakini maskini kiburi hicho. "Loo, unataka kusema, kwetu sisi wanawake, itatulazimu kuacha nywele zetu zikue?" Vema, hilo ndilo alilosema. "Ati itatulazimu kuacha kuyapaka rangi makucha yetu, ama kujipodoa?" Hilo ndilo Yeye alilosema. "Vema, unafikiri kundi langu la kushona lingesema nini? Wataniita wa mtindo wa kale." Vema, kaa tu na kiburi chako. Endelea. Yeye atasimama mlangoni, huo ndio umbali tu anaoweza kwenda.

170 Lakini unapokuwa tayari kuufungua mlango huo, umwache aingie ndani, Yeye atausafisha kwa ajili yako. Kaptura zitatupwa nje hapa kwenye pipa la takataka, navyo vipodozi vitarudi kwenye pipa la takataka, na kinyozi atakufa kwa njaa endapo hana kazi nyingine ila ni kukata tu nywele za wanawake, kwa mwaminio halisi.

171 Sasa unasema, "Hilo halijalishi!" Loo, naam, linajalisha, pia. Hilo ndilo Biblia ililosema. Hiyo ni kweli. Unaona, kuna neno dogo pale, ambalo wewe hutaki Yeye aingilie.

"Vema, mchungaji wangu!"

172 Sijali yale mchungaji aliyosema. Hilo ndilo Biblia ililosema, "Ni aibu kwa mwanamke kufanya hivyo."

173 "Vema," unasema, "inatupasa utufundishe mambo, Ndugu Branham, ni jinsi ya kumpata Roho Mtakatifu, na jinsi ya kuwa *hiki, kile*." Utaendaje kujifunza algebra kama hujui ABC zako? Hata hujui jinsi ya, ya kutenda, kuonekana kama mmoja, kuvaa kama mmoja. Ni aibu kuwaona wanawake hawa mtaani siku hizi.

174 Niliingia mahali fulani jana, wakati, loo, baadhi ya wahuni waliopotoka waliingia. Wao, wanaume hao walikuwa na nywele zilizofikia machoni mwao, zilizoshuka na kuning'inia mgongoni mwao, kama legotadi, kama zile zinazovaliwa na watoto wadogo wakienda shuleni, wamevaa maskini viatu vikubwa mno vichakavu, midomo nusu wazi. Ungeweza kujua walikuwa ni wahalifu. Nao waliingia pale namna hiyo, wakasema, "Sisi ni Wafaransa."

175 Ni nani ulimwenguni angalimwajiri mtu kama huyo kwenye biashara yake? Wanapataje riziki yao? Nami niliona baadhi ya wavulana wa kweli wameketi pale . . . Walitoka kwenye kile chuo kikuu huko chini, hawa wahuni walitoka huko, ama nafikiri wanajiita *vijidudu* ama *mende*, ama kitu kama hicho, baadhi ya upuuzi huo unaotoka Uingereza. Na halafu humo ndani jinsi hiyo, ni nani angemwajiri mtu kama huyo amfanyie kazi? Je! ungeweza kumweka mtu kama huyo kwenye biashara yako, enyi wafanya biashara? Kama ungemwajiri, wewe ni, kuna jambo fulani, hujaukaribia Msalaba vya kutosha bado.

176 Waangalie wanawake hawa huko nje mtaani, na ni fedheha! Pengine ni maskini wanawake wasio na hatia waliovaa nguo hizi fupi, unaona, vema, ni fedheha, jinsi wanavyoonekana. Vema, mnasema, "Mbona, ewe mwanamke, unafanya uzinzi."

177 Wao wanasema, "Ngoja kidogo hapa, ewe kijana! Mimi ni mwadilifu tu kama mimi . . . " Huenda hiyo ikawa ni kweli, katika mawazo yako mwenyewe. Na huenda ikawa ni kweli, kuthibitishwa hata na uchunguzi wa daktari, huenda ukawa hivyo.

178 Lakini, kumbuka, kwenye ile Siku ya Hukumu, utajibu kwa kufanya uzinzi. Yesu alisema, "Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake," nawe ulijianika kwake. Unaona jinsi ibilisi amewapofusha? Ni fedheha. Ni aibu. Unaona, wao—wao wana pepo. Pepo ndiye anayefanya jambo hilo. Ni pepo mchafu.

179 Lakini Roho Mtakatifu halisi atamfanya mwanamke kuvalia vizuri na kuonekana mtakatifu.

180 Mke wangu aliniambia, wakati mmoja. Tulikuwa tukishuka mtaani, nasi tukakutana na mwanamke aliyevaa rinda, huko nchini mwetu. Lilikuwa ni jambo la kigeni sana, unaona, hakukuwako na wapentekoste wengi sana zamani hizo. Kwa hiyo, tunaona ya kwamba alikuwa amevaa rinda. Basi akasema, "Billy," akasema, "Ninawajua baadhi ya wanawake hao. Wanaimba kwenye kwaya huku chini kwenye makanisa haya."

Nikasema, "Hakika."

Kasema, "Vema, ati nao wanadai kwamba ni Wakristo?"

Nikasema, "Mpenzi, angalia. Unaona, sisi si ninii . . . "

Kasema, "Kwa nini watu wetu?"

Nikasema, "Angalia, mpenzi, sisi si wa jamii yao—yao hata kidogo."

Akasema, "Ati nini?" Kasema, "Hao ni Wamarekani."

Nikasema, "Naam, bali sisi sio hao."

Akasema, "Ati sisi sio?'

Nikasema, "La."

181 Nikasema, "Ninapoenda Ujerumani, ninapata roho ya Kijerumani. Nilipoenda Ufini..." Kule kwenye sauna, wengi wenu Wafini mnajua, wanawake ndio wanaowaogesha wanaume. Kwa hiyo, hiyo ni roho tu ya Kifini. Watu wazuri sana, lakini, unakuta, kokote uendako, unapata roho ya kitaifa.

182 Hebu nenda kanisani na umwangalie mchungaji, iwapo yeye ni mshamba kweli na anapiga makelele, kusanyiko litakuwa vivyo hivyo. Mnaona? Wanachukua roho ya mmoja kwa mwingine badala ya Roho Mtakatifu.

183 Hiyo ndiyo sababu tuna mafundisho mengi sana yaliyopotoshwa ya Biblia. Badala ya kurudi kwenye ramani, wao wamechukua roho ya madhehebu fulani. Unaona? Bali Neno ni geni kwao tu kama lilivyokuwa katika siku ambazo Yesu alikuja, akiitangaza Injili halisi na ya kweli. Wao walisema, "Yeye ni ibilisi. Yeye ni Beelzebuli." Unaona? Lakini hapo unalipata.

184 Naye akasema, "Vema, kumbe, sisi si Wamarekani, sisi ni nani?"

185 Nikasema, "Ufalme wetu ni wa huko Juu." Unaona, sisi ni huru, tumezaliwa mara ya pili. Ufalme wa Mungu umo ndani yenu. Unaona, unatenda kama huko Juu, ninyi ni wajumbe wa kutoka Huko. Nikasema, "Sisi ni raia hapa, tukiishi hapa katika mwili. Lakini, roho zetu, sisi ni wasafiri na wageni." Sisi ni wageni kwa ulimwengu sasa, hata na taifa letu wenyewe, kwa kuwa tumeukubali mwaliko wakati ulipoubisha moyo wetu, tupate kuwa sehemu Yake, Neno Lake. Nalo Neno linatuimarisha, linatufanya tuishi na linatufanya kutenda kama Wakristo.

186 Zamani za kale, huko Kusini, hadithi ndogo. Kulikuwako na mfalme...ama, mnunuzi. Waliuza watumwa. Huo ulikuwa ni ule wakati wa—wa ubaguzi, nao walikuwa na watumwa huko Kusini. Walikuwa...Wangepitia kule na kuwanunua, kama tu vile ungelinunua gari la mtumba, kutoka mahali lilipoegeshewa.

187 Sasa, mimi ni muunganishi, kweli kabisa...ninamaanisha mbaguzi. Mimi ni mbaguzi. Kwa sababu, sijali wanabishana jinsi gani, huwezi kuwa Mkristo na uwe muunganishi. Hiyo ni kweli kabisa. Mungu hata huyatenganisha mataifa Yake. Huwatenganisha watu Wake. "Tokeni kati yao!" Yeye ni... Yeye ni mbaguzi. "Hata msininii...Msiguse vitu vyao vilivyo vichafu!" Yeye aliwavuta Israeli, hiyo jamii ya Kiyahudi, kutoka kwenye kila, jamii zote ulimwenguni. Yeye ni mbaguzi.

188 Lakini siamini ya kwamba mtu yeyote anapaswa kuwa mtumwa. Mungu alimfanya mwanadamu; mwanadamu akawafanya watumwa. Siamini mtu anapaswa kumtawala mwingine, jamii yoyote, rangi yoyote, wala chochote kile.

189 Bali kuna ubaguzi, Bibi-arusi wa Kristo ametengwa na makanisa mengine yote, na hilo ni kweli kabisa: kanisa la kawaida, na Kanisa la kiroho; kanisa la kimwili, Kanisa Neno.

Imekuwa hivyo daima. "Yesu alikuja kwa walio Wake, walio Wake hawakumpokea; bali wote waliompokea!"

190 Kwa hiyo huyu, walikuwa ni wanunuzi, madalali wanapitia pale na kuwanunua hawa watumwa. Wakati mmoja palikuja mmoja kwenye shamba kubwa, naye akawaangalia. Hao watumwa walipigwa sana, na kila kitu, unajua. Walikuwa mbali na makwao; kamwe wasingerudi tena. Nao Makaburu, Waholanzi, walikuwa wameenda huko na kuwachukua mateka, wakawaleta hapa na kuwauza. Nao hawatamwona baba tena, mama tena, kamwe hawatawaona watoto wao wachanga tena. Waliwazalisha mmoja kwa mwingine; walimchagua mwanamume mkubwa, wakamzalisha na mwanamke mkubwa, mbali na mkewe, wapate kuwazaa watumwa wakubwa. Loo, Mungu atawafanya wawajibikie hilo siku moja! Hiyo ni kweli. Hilo si sawa.

191 Kama vile Abraham Lincoln alivyosema wakati mmoja, wakati aliposhuka kwenye mtumbwi huko New Orleans, akachukua kofia yake ya bomba la stovu . . .

192 Aliwaona wanegro watatu ama wanne wadogo, wakati akishuka kuja, wamesimama pale miguu peku, ambapo walikuwa . . . Ng'ombe alikuwa amelala na ku—kuondoa jalidi sakafuni, walikuwa wamesimama baada ya kuwaingiza ng'ombe. Miguu yao midogo imepasuka, inatokwa na damu. Walikuwa wakiimba, "Una viatu, nina viatu, na watoto wote wa Mungu wana viatu."

193 Alipotoka kwenye mashua hiyo kule chini, akaenda kwenye zizi la fahali, kulikuwako na mnegro mkubwa mno amesimama pale, wakimpiga mijeledi, kuufanyia moyo wake majaribio. Nao wanamkimbiza huku na huku mtaani, na mjeledi nyuma yake; kisha wanauchunguza moyo wake, waone kama alikuwa sawasawa. Maskini mke wake amesimama pale, watoto wawili ama watatu mkononi mwake namna *hiyo*; wamuuze, wakamzalishe na mwanamke mkubwa zaidi. Maskini Abraham Lincoln akachomeka hilo chini ya kofia yake . . . kofia yake chini ya mkono wake, namna *hiyo*, na kuipiga ngumi yake, akasema, "Hilo ni jambo baya! Na siku moja nitalilipua hilo, kama likinigharimu maisha yangu." Na huko, kwenye jumba la makumbusho huko Chicago, lipo vazi lililo na damu, lililomweka huru mtumwa huyo kutoka kwenye kitu hicho.

194 Nami ninasema ya kwamba dhambi na kadhalika ni makosa! Mungu na anisaidie kuipiga vita, na wahudumu wengine wote wa Injili. Tumezaliwa huru, watoto wa Mungu. Hatuna shughuli na kanuni yoyote ya imani ama dhehebu kutuingiza kwenye Baraza la makanisa Ulimwenguni. Tumezaliwa watu huru, katika Roho Mtakatifu. Tunayo haki. Tulitoka kwenye upuuzi kama huo, tupate kuwa wapentekoste. Hiyo ni kweli. Sasa tuko huru. Haitupasi kufungwa kwenye mambo hayo tena.

195 Lakini mnunuzi huyu alisema, akiwaangalia watumwa wake, mia moja ama kitu kama hicho, wa hao, katika shamba kubwa, akasema, "Aisee!" Maskini jamaa mmoja pale, haikuwabidi kumpiga mijeledi; kifua mbele, na kidevu chake amekibenua juu, moja kwa moja kazini! Kasema, "Aisee! Ninataka kumnunua."

196 Akasema, "Loo, la!" Mwenyewe akasema, "Huyo hauzwi. A-ha."

Akasema, "Vema, hivi yeye ni mtumwa?"

Kasema, "Ndiyo."

197 Akasema, "Vema, ni kitu gani kinachomfanya tofauti sana?" Kasema, "Je! unamlisha tofauti?"

Akasema, "La, wote wanakula huko kwenye manchani, pamoja."

Kasema, "Hivi yeye ndiye bosi wao?"

Kasema, "La, yeye ni mtumwa tu."

"Vema," kasema, "ni kitu gani kinachomfanya kuwa tofauti?"

198 Kasema, "Unajua, hilo lilinishangaza, mimi mwenyewe. Lakini," kasema, "unajua, huko katika nchi ya uenyeji wake wanakotoka, huko Afrika, baba wa mvulana huyo ni mfalme wa kabila moja. Na ingawa yeye ni mgeni, yeye hutenda kama mwana wa mfalme."

199 Loo, nikawazia, ni jambo la jinsi gani kwa Ukristo! Enyi wanawake, achaneni na huko kuvaa nguo hizo jinsi hiyo! Enyi wanaume, acheni huko kutoa hiyo mizaha michafu na upuuzi huo wote! Sisi ni wana na binti za Mfalme. Vaeni kama malkia, vaeni kama ma—mama wa heshima. Fanyeni kama muungwana, msiache nywele zenu zikue jinsi *hii*. Biblia ilisema, "Ni kosa (maumbile yanawafundisha) kwa mwanamume kuwa na nywele ndefu. Na ni fedheha na si jambo la kawaida kwa mwanamke hata kuomba huku amekata nywele zake." Na haya je? "Ni—ni chukizo kwa mwanamke kuvaa vazi limpasalo mwanamume." Mungu mkuu asiyebadilika habadiliki. Lakini hata hivyo siku hizi yamelegea tu kama taifa letu lilivyolegea. Aibu! Hebu tutende kama wana na binti za Mungu. Hebu na tuishi jinsi hiyo. Sisi ni, sisi ni wana wa Mfalme. Ndivyo tulivyo. Ndivyo tulivyo. Sasa hivi lundo hili la machafuko na uchafu, hapa, watu wakijiita "Wakristo" na wangali wakitenda hivyo!

200 Lakini kumbukeni, tulipigiwa hodi siku moja, nasi tukamfungulia aingie, majivuno na kila kitu yakaondoka. Amina. Sijali wananiita nini!

Loo, nafikiri mimi kidogo ni wa mtindo wa kale,
Lakini Mwokozi wangu alikuwa wa mtindo wa kale, pia.

201 Hiyo ni kweli? Mmeusikia wimbo huo. Iweni wa mtindo wa kale! Usijaribu kujilinganisha na mtu mwingine. Yeye ndiye Mfano wako. Jaribu uwe kama Yeye, Naye Roho aliye ndani yako atakusaidia kufanya hivyo. Atayafanya maisha yako kama Yake.

202 Naam, kuna mlango hapo. Ninataka kutaja mlango mwingine. Ninafungwa sana. Kuna mlango mwingine hapo, karibu tu na mlango huo, ukizunguka kwenye mkono wa kuume, na mlango huo ni mlango wa maisha yako ya kibinafsi. Loo! Loo, hutaki auchezee huo. "Sasa, kama nikitaka kutoka niende kwenye karamu ndogo ya kokteli, inakuhusu nini? Ni kanisa gani litakaloniambia nitakalofanya?" A-ha, haya basi, unaona. "Ati fungu la kumi la mshahara wangu? Ni nani atakayeniambia cha kufanya? Hayo ni maisha yangu ya kibinafsi! Ninachuma fedha hizi. Nina maisha yangu mwenyewe. Nitavaa kaptura nikipenda. Hiyo ni haki yangu mwenyewe ya Kimarekani." Hiyo ni kweli. Hakika. Kweli.

203 Bali kama wewe ni mwana-kondoo, wala si mbuzi, unaona Yeye anawatafuta wana-kondoo. Watatenganishwa siku moja.

204 Kondoo ana sufu. Hicho ndicho kitu cha pekee alicho nacho. Wala hawezi kutengeneza sufu hiyo. Hatuombwi kutengeneza tunda la Roho, bali *kuzaa* tunda la Roho. Na mradi tu yeye ni kondoo, atazaa. Haimbidi kutengeneza. Zile tezi na kila kitu ndani yake ni kondoo, ataota sufu kwa kuwa ndani yake mna tezi na adrenalini na kadhalika zinazohitajika kufanya sufu.

205 Na wakati unapokuwa u Mkristo, utaambatana na Neno. Sijali mtu mwingine yeyote anasema nini. Haikubidi kuigiza chochote, na kushusha chochote, kuvuta, kusukuma. Wewe ni Mkristo. Unazaa tu tunda la Roho moja kwa moja. Unaona? Unaona, na hivyo ndivyo ilivyo. Unaona?

206 Lakini, watu siku hizi, hawataki uyachezee maisha yao ya binafsi.

207 Jambo pekee unalofanya, fungua tu kila mlango hapo, sasa sema, "Karibu ndani, Yesu." Angalia linalotukia. Unapoona katika Kitabu, unapaswa kufanya *hili*, utalifanya. Kwa nini? Kwanza, wewe ni kondoo, basi.

208 Bali kama unataka tu kuketi, kumweka Yeye mlangoni, useme tu, "Nimejiunga na kanisa. Mimi ni mwema tu kama ulivyo wewe. Unaona, nilimkubali Kristo." Labda hilo ndilo tu ulilofanya. Lakini je! ulimfanya Yeye *Bwana*? Unaona?

209 Sasa, Bwana hawezi kuweka tu chini Kitabu cha sheria na kusema Neno, halafu arudi na kulikana. Na kama unasema una Roho Mtakatifu, nayo Biblia inasema ufanye jambo fulani, nawe unasema, "Loo, siliamini *Hilo*." Hebu kumbuka tu, roho hiyo iliyo ndani yako si Roho Mtakatifu, maana Yeye hawezi kujikanusha. Hiyo ni kweli. Hawezi kujikanusha Mwenyewe. Yeye aliliandika hilo Neno, Naye huliangalia, apate kulitimiza. Unaona? Kwa hiyo si nanii Mtakatifu . . .

210 Ni roho, sawa. Huenda ikawa ni ro—roho ya kanisa. Huenda ikawa ni roho ya mchungaji. Huenda ikawa ni roho ya ulimwengu. Huenda ikawa. Sijui ni kitu gani, lakini, hata iwe ni nini, huenda ikawa ni roho ya kimadhehebu, "Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mpentekoste. Mimi ni *hili*." Hiyo ni Pentekoste.

211 Sasa kumbukeni, hebu nilinyoshe; pentekoste si dhehebu, pentekoste ni tukio unalopata. Ninyi Wamethodisti, Wabaptisti, Wakatoliki, na wote, mnaweza kupata tukio la pentekoste. Huwezi kujiunga na pentekoste, maana hakuna njia ya kujiunga nayo.

212 Nimekuwa kwenye familia ya Branham kwa miaka hamsini na mitano. Mnajua, kamwe hawakuniomba niwe Mbranham. Nilizaliwa, Mbranham.

213 Na hivyo ndivyo ulivyo Mkristo, unazaliwa Mkristo. Hiyo ni kweli, sasa.

214 Loo, hayo maisha ya kibinafsi! "Loo, nakwambia, mchungaji wangu huenda kwenye madansi haya, nasi tunanengua. Wanayo." Vema. Unaona? "Usije ukiniambia yale ninayoweza kufanya na yale nisiyoweza kufanya." Vema, unaona, hutamruhusu Yeye aingie.

215 Hebu mwache tu aingie ndani wakati mmoja, kisha urudi kwenye kunengua ama kwenye roki, ama chochote unachoenda kufanya, uone kile unachoweza kufanya. Huwezi kulifanya. Hebu mwache Yeye aingie wakati mmoja, kisha uanze kuvaa jozi ya kaptura, baadhi yenu wanawake.

216 Ninajua ninawacheleweshа sana, bali ninataka kusema jambo moja zaidi, kama ni sawa, kuhusiana na hili.

217 Nadhani, mkutano ulio mkubwa sana ambao Bwana ameniruhusu kumfanyia ulikuwa huko Bombay, ambako nilikuwa na karibu watu elfu mia tano, lakini, na elfu mia mbili na kitu hu—huko Afrika, Durban, kwenye uwanja wa mbio za farasi. Alasiri hiyo, nilisema, baada ya wao kuona jambo la ajabu mno ambalo Bwana wetu mwenye neema alishuka na kulifanya, nilisema, "Wamishenari waliwafundisha Neno, bali Neno limehuishwa na kufanywa hai. Kile asemacho hakina budi kuwa hai." Na—na halafu wakati ulipofanyika uponyaji elfu ishirini na tano wakati mmoja, na lundo baada ya lundo la viti vikuukuu kule; ombi moja tu rahisi, walikuwa wamemwona Roho Mtakatifu akininii tu...Hao watu ambao hata hawakujijua walikuwa ni akina nani na mahali walikotoka, hilo tu ndilo walilotaka kuona. Mnaona?

218 Ndipo nikauliza, "Ni wangapi wanaotaka kumpokea Kristo?" Kulikuwako na elfu thelathini waliosimama kwa miguu yao, wenyeji waliovaa mablanketi, waliobeba sanamu.

219 Daktari Bosworth, Daktari Baxter na hao wengine, wakaanza kulia. Ndipo Ndugu Bosworth akaja upesi, kasema—kasema, "Ndugu Branham, hii ndiyo siku yako ya kutawazwa."

220 Ndugu Baxter akasema, "Ndugu Branham, sijui, nafikiri walimaanisha uponyaji wa kimwili."

221 Mvulana huyo alikuwa akitambaa kwa mikono na magoti yake. Naye Roho Mtakatifu akamwambia mahali alikotoka, kilichompata, kasema, "Utazungumza. Wazia juu ya ndugu yako, yeye yuko kwenye umbali wa karibu nusu maili kule nyuma. Alikuwa amebebwa na mbuzi wa manjano, ndipo akaujeruhi mguu wake." Nikasema, "Lakini, BWANA ASEMA HIVI, ameponywa." Huyu hapa huyo mvulana anakuja, amebeba mikongojo mikononi mwake, namna *hiyo*. Nalo lilichukua kama dakika ishirini kwa wanamgambo kuwanyamazisha.

222 Ndipo mvulana huyu, akitambaa kwa mikono na miguu yake, namna *hiyo*, chini, hata asingeweza kuinuka, yu uchi. Loo, jamani, kitu cha kuchukiza jinsi hiyo! Alidhani alikuwa akija kule juu kwa watalii, unajua, kwa namna fulani kucheza da—dansi la porini. Ndipo nikaushika ule mnyororo na kuutikisa. Nikasema, "Kama ningaliweza kukisaidia maskini kiumbe kile, wala nisikisaidie, ningekuwa ninii. . .nisingestahili kusimama nyuma hapa. Lakini," nikasema, "siwezi kumsaidia. Lakini sasa nina karama ndogo, ninaweza tu kuitia gia, lolote Bwana asemalo."

223 Basi wakati Bwana alipoonyesha, alipomwambia yeye alikuwa ni nani, kasema, "Mama na baba yake wameketi mle ndani, wao ni Wazulu." Kisha kasema, "Hao ni wembamba, si kawaida." Mzulu atakuwa na ratili mia tatu wastani, kwa kila mwanamume. Kwa hiyo basi kasema, "Hao si wa kawaida. Lakini mvulana huyu alizaliwa katika nyumba ya Kikristo, kwa kuwa kwenye ninii yake. . .upande wake wa kuume, unapoingia mlangoni, ipo picha ya Kristo, kwenye kibanda kidogo cha nyasi." Na hilo lilikuwa ni kweli kabisa. Mama na baba yake wakasimama. "Na *hilo* ndilo jina lake." Hivyo ndivyo alivyokuwa, na kila kitu. Wasingeweza kuelewa. Niliangalia nyuma nikamwona amesimama, katika ono pale, amesimama wima amenyooka kabisa alivyoweza kuwa. Hajapata kusimama, maishani mwake, alizaliwa jinsi hiyo. Nikasema, "Bwana Yesu anamponya."

224 Hata hakuwa na akili timamu, akijaribu kwenda, "uha, ba, ba, ba," namna hiyo.

225 Ndipo nikaushika mnyororo huo, nikautikisa namna *hiyo*. Nikasema, "Yesu Kristo, mwanangu, amekuponya. Simama kwa miguu yako." Hapo akasimama. Machozi yakitiririka, na kupitia kwenye tumbo lake jeusi, wakati alipokuwa akishuka chini namna hiyo. Niliwaona wenyeji elfu thelathini wanaovaa mablanketi wakiyatoa maisha yao kwa Yesu Kristo.

226 Wakati nikiwa kwenye Klabu ya Kiwanis, nilisema sasa . . . Nao waliniambia nitakuwa "mtakatifu anayejifingirisha" wakati nilipoliacha kanisa la Kibaptisti, kusudi nipate kushirikiana na watu wote. Wao walisema, "Vema, utakuwa mtakatifu anayejifingirisha," niliketi. Kundi la ndugu zangu wa Kibaptisti walisema. Nikasema, "Mmewatuma wamishenari huko ndani, kwa miaka mia moja na hamsini iliyopita, niliwakutaje? Wangali wanabeba sanamu." Nikasema, "Bali nguvu za kufufuka kwake Yesu Kristo, elfu thelathini walimpokea Kristo katika wakati mmoja."

227 Sasa ninataka kuwaambia ninyi wanawake, mnajua kilichowapata wanawake hao? Nikasema, "Papo hapo mahali mmesimama, Roho Mtakatifu atawajaza." Ndipo wakati walipoinua mikono yao kumpokea Kristo kama Mwokozi wao, na wakati walipoondoka hapo; uchi, sasa, hakuna kitu ila kipande kidogo sana, kijitambaa, hapo mbele. Na wakati walipoondoka pale, walikunja mikono yao namna *hii*, kwa kuwa walikuwa mbele ya mwanamume, wakiisha kumpokea Kristo.

228 Sasa tunawezaje sisi, enyi dada, tunawezaje katika taifa hili ambapo tunadai tunaamini na tu Wakristo, na kila mwaka wao wanazivua zaidi? Wakati, mtu huyo hata kamwe hajalisikia Jina la Kristo, bali ndio kwanza wampokee moyoni mwao. La, usingeweza kuwaambia walikuwa uchi, hawakujua hilo. Bali walijifunika namna *hii*, wapate kuondoka. Siku moja, ama mbili baadaye, ungekutana nao wamevaa nguo, za namna fulani. Loo, jamani!

229 Kuna kitu kasoro mahali fulani. Ni kuvurugika kwa theolojia. Nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo, kama Yeye alivyomfanyia yule mtu aliyeitwa "Jeshi," tulimkuta amevaa nguo na akiwa na akili zake timamu. Ndipo nikaanza kuamini ya kwamba ni pepo juu ya watu ambaye anawasukuma kwenye Umarekani na Ufaransa, na kila namna ya mambo ya ulimwengu na ukanisa. Lakini hebu wakati mmoja wamjie yule Bwana, na wahisi ule mbisho mlangoni, watavaa nguo na kutenda kama wanawake na wanaume, nao watakuwa ni Wakristo waliozaliwa mara ya pili. Amina. Naam.

230 Sasa nimemaliza, saa sita kasoro dakika ishirini, da— dakika chache tu, hebu niruke mengine. Hebu kidogo, baadhi ya Maandiko, ningependa kufungua mlango mmoja zaidi. Litakuwa sawa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

231 Mlango unaofuata, wa kuingia pale, ni imani. Unaona, maisha yako ya kibinafsi . . . mlango wa kiburi, maisha yako ya kibinafsi, sasa hebu na tufungue imani. Mlolongo mzima tu wa hiyo, unaona, bali hebu tuingie katika imani.

232 Unajua, siku moja nilikuwa hosptalini na mwanamke mmoja alikuwa akifanyiwa upasuaji. Alinipigia simu, akasema, "Ndugu Branham, mimi nimerudi nyuma. Ungeweza kuniombea?"

233 Nikasema, "Naam, mama, ningefurahia kufanya hivyo." Nikasema, "Ati umerudi nyuma?"

"Ndiyo."

234 Nikasema, "Sasa hebu tungojee tu dakika moja. Hebu nikusomee Maandiko."

235 Kulikuwako na mama aliyelala pale kitandani, akaniangalia, kiajabu sana; yeye, na mwanawe mwenye umri wa kama miaka ishirini, Riki wa kawaida, naye amesimama pale akiniangalia namna hiyo.

236 Ndipo nikasema, "Naam, mama," nikasema. Nikamsomea Maandiko, "Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji. Zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa nyeupe kama sufu." Na nilipomsomea hayo, nilisema, "Kama umetangatanga, unaona, umemwacha Mungu, bali Mungu kamwe hakukuacha, la sivyo usingekuwa ukiniita." Akaanza kulia. Nikasema, "Tutaomba."

237 Mama huyo kwenye kitanda hicho kingine, akasema, "Ngoja kidogo! Ngoja kidogo hapo!"

Nikasema, "Naam, mama?"

Akasema, "Rudisha pazia hilo!"

Nami nikasema, "Hivi wewe si Mkristo?"

Akasema, "Sisi ni Methodisti!"

238 Nikasema, "Vema, hilo lina uhusiano gani nalo? Unaona, hiyo si zaidi ya kusema ulikuwa ninii—ulikuwa mwana farasi, kama ulikuwa kwenye zizi la nguruwe, unaona." Nikasema, "Hilo halimaanishi kitu." Unaona?

239 Lakini, unaona, hapo ndipo imefikia, huko kujidai. "Hilo ni kinyume na imani yetu!" Nikasema ninii . . . "Hatutaki uponyaji wa kiungu kanisani mwetu, ama upuuzi kama huo." Mnaona, mnaona ninalomaanisha? Mnaona, hawataufungua mlango huo. "Hilo ni kinyume na imani yetu."

240 Kuna Imani moja tu. "Imani moja, Bwana mmoja, ubatizo mmoja." Ile Imani!

> Imani yangu inakuangalia,
> Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,
> Mwokozi wa Kiungu;
> Sasa nisikie niombapo,
> Ondolea mbali kutokuamini kwangu kote.

241 Dhambi! Dhambi, kuna dhambi moja tu, hiyo ni kutokuamini. Mtu anayekunywa pombe si mwenye dhambi. Unaona, hiyo—hiyo—hiyo, unaona, siyo dhambi. Si ninii—kunywa pombe si dhambi. Kufanya uzinzi si dhambi. Kusema

uongo, kuiba, hiyo si dhambi. Hayo ni matokeo ya kutokuamini. Kama ungalikuwa ni mwaminio, usingefanya jambo hilo, unaona.

242 Kuna mbili tu, wewe ni asiyeamini ama ni mwaminio, unaona, mmojawapo. Hufanyi mambo haya yote na taratibu za kidini namna hiyo, ni kwa sababu tu wewe si mwaminio; kama wewe ni mwaminio, Neno ndilo unaloamini, maana Kristo Ndiye Neno. Unaona? Na kwa hiyo wewe ni asiyeamini tu kwa kuwa unaamini mapokeo fulani, ama mafundisho fulani ya sharti ambayo yameongezewa kwenye Biblia, ama kitu fulani, nayo madhehebu huyafanya. Bali mwaminio wa kweli hudumu moja kwa moja na Neno hilo. Na Mungu hufanya kazi moja kwa moja kupitia kwenye Neno hilo, moja kwa moja kulifanya litimie, katika kizazi hiki tunachoishi.

243 Na sasa angalieni, nanyi mnasema, "Loo, mimi . . . Ndugu Branham, Bwana . . ." Vema, hilo ni sawa, kulikuwako na Wafilisti wengi wasiotahiriwa walioondoka wakati mmoja, pia. Na kundi la Wamisri likajaribu kumfuata Musa kuvuka Ba— Bahari ya Shamu, bali hatimaye . . . "Kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa, vema, tunakuta jambo lile lile katika siku ya mwisho," Biblia ilisema.

244 Sasa mbele kidogo tu. Yesu alisema hapa, katika wakati huu—huu, "Kwa kuwa unasema ya kwamba, 'Mimi ni tajiri, na nimejitajirisha.'" Angalieni tu jinsi tulivyo siku hizi, kanisa tajiri sana lililopata kuwako! Na, vema, unajua, ninyi Wapentekoste mngekuwa bora zaidi kama mngalikuwa huko nje mkiwa na tari, huko pembeni, kama vile baba na mama zenu walivyokuwa. Lakini mna makanisa bora kuliko hao wengine sasa, yanayopanuka upesi zaidi ulimwenguni; bali yu wapi yule Roho wa Mungu aliyekuwa miongoni mwetu? Mlikiacha kitu halisi. "Kwa kuwa unasema, 'Mimi ni tajiri.'"

245 Kumbukeni, hii ni pentekoste linayoizungumzia, maana wakati wa Pentekoste ndio wakati wa mwisho. Mnaona, uamsho huu wote ambao tumekuwa nao, hakuna dhehebu lingine litakaloibuka. Hakutakuwako. Huu ndio mwisho. Ngano imekomaa sasa. Imepitia kwenye majani, na ubua, na ganda, na imefikia kwenye ngano sasa. Mnaona, hakutakuwako na lingine. Walianzisha maskini Mvua ya Vuli, bali liliporomoka tu; kitu kingine chochote kitaporomoka. Wataporomoka. Hii ni ngano inachipuka. Angalieni.

246 "Na kwa kuwa unasema, 'Mimi ni tajiri, na nimejitajirisha, sina haja ya kitu,' nawe hujui ya kuwa wewe ni mnyonge, mwenye mashaka, kipofu, uchi, wala hujui; nakupa shauri . . ." Loo, jamani! "Ninabisha mlangoni pako." [Ndugu Branham anagonga kwenye kitu fulani—Mh.] "Laodikia, nabisha mlangoni penu, na kuwashauri mje Kwangu, na—na mkanunue

dhahabu iliyosafishwa kwa moto; nguo nyeupe, uchi wenu usije ukaonekana."

247 Yaondoeni mambo haya, mkavae kama iwapasavyo, unaona, haki ya Kristo, Maneno. Sio haki yangu; haki Yake!

248 "Na pia ninawashauri m—mje, mpate dawa ya macho, mkayapake macho yenu, mpate kuona. Dawa ya macho!"

249 Mimi ni Mkentaki. Nilizaliwa huko chini milimani, nasi tulikuwa na maskini mahali padogo huko darini. Nasi watoto tulikuwa tumetengeneza ma—maskini ngazi ya ufito, tuliyopanda nayo kila usiku. Nasi tukalala. Iliwabidi kutufunika kwa kipande cha turubai wakati barafu ilipoanguka. Vema, nyota, mbao mbovu chakavu za mlowe . . .

250 Ni wangapi wanaojua mbao za mlowe za kuezeka ni kitu gani? Vema, ndugu, kwa nini sikuvaa ovaroli zangu huku juu? Niko nyumbani kabisa, mnaona. Vema, mbao chakavu za mlowe za kuezeka!

251 Ni wangapi wanaojua mto wa manyasi ni kitu gani? Sasa mnajua nini! Nilifikiri nilijisikia kubarikiwa sana kuhusu jambo fulani. Vema, nadhani niko nyumbani kabisa sasa. Hilo ni zuri. Wala sikujua kitu kingine mpaka miaka michache tu iliyopita.

252 Ni wangapi wanaojua taa ya kale ni nini, chemli ya kale, mwajua? Hiyo ilikuwa ni maskini mwezi wa kale, na bundi kando yake. Walikuwa na ule mkono ulio mdogo zaidi nyumbani, iliwabidi kusafisha gudulia hilo la kale, mwajua. Nilikuwa na mazoea ya kuchukua bamba la kurushia la kale, nalo lingenirushia kote; kwa hiyo nikachukua hiyo taa ya chemli na kuirudisha kule, isije ikarushia. Naam, kweli.

253 Sasa, babu yangu alikuwa ni mtegaji. Mama ya mama yangu alitoka kwenye ardhi iliyotengwa. Alimwoa msichana wa Kihindi kutoka kwenye ardhi iliyotengwa ya Wacherokee kule Kentucky na Tennessee, mnajua ni wapi, kwenye bonde la Cherokee. Na, wao, yeye a—aliwinda na kutega, wakati wote, hivyo—hivyo ndivyo alivyojipatia riziki yake.

254 Na sisi watoto tumelala pale, mbona, wakati mwingine kulikuwa na baridi sana. Na huo upepo ukipitia pale, tungeshikwa na baridi machoni mwetu, na—na macho yetu yangefungamana usiku, mwajua. Mama aliyaita "matongo." Sininii—sijui hiyo ni nini, bali baridi ingeingia machoni mwako, nayo yangeshikwa na baridi. Ndipo angesema, "Una matongo machoni mwako," kwa sababu ya—ya, mwajua, upepo ukizungukazunguka kupitia pale, huo upepo wa baridi unakuja usiku. Macho yetu yangevimba hata yakafunga.

255 Naye mama angeenda pale kwenye ile ngazi, asubuhi, wakati alipokwisha kupika biskuti. Angeweka molasi ya mtama mezani. Naye angesema, "Billy!"

Ningesema, "Naam, mama?"

"Wewe na Edward shukeni chini."

256 "Mama, siwezi kuona!" Nikamwita ndugu yangu, tulimwita "Humpy." Nikasema, "Hawezi kuona, pia. Unaona, macho yetu yalikuwa yameingia matongo."

Angesema, "Vema, hebu kidogo."

257 Na babu, wakati akimshika kuuni. Ni wangapi wanaojua rakuuni ni kitu gani? Huyo ndiye, naye angeninii . . . Angemshika kuuni, angemtoa mafuta na kuyaweka kwenye kopo. Na hayo mafuta ya kuuni yalikuwa ni mponya yote katika familia yetu. Wangetupatia hayo kwa ajili ya mafua makali, pamoja na terafini ndani yake, na mafuta ya makaa. Tungeyameza kwa ajili ya homa ya koo. Kisha angeyachemsha hayo mafuta ya kuuni, angekuja na kuyasugua macho yetu, nayo macho yetu yangefunguka. Mnaona, mafuta ya kuuni ndiyo yaliyofanya jambo hilo. Mnaona?

258 Sasa, ndugu, dada, tumepitia kwenye kipindi cha baridi, kanisani. Hiyo ni kweli, upepo mwingi wa kidini umepitia humu, kila mtu ameshikwa na mafua. Watu wengi wamefumbwa macho kabisa, na kuna Baraza kuu la Makanisa Ulimwenguni linalokuja, huku, litamlazimisha kila mmoja wenu ndani yake. Wanaliacha hilo Neno, makundi yetu yanaliacha. Mimi ninawajibika kwa Ujumbe; sio kuwa tofauti, bali ni kwa sababu ya upendo. Upendo husahihisha. Rudini! Kaeni mbali na kitu hicho! Ninyi ndugu wahudumu, sijali yale makundi yenu yafanyayo, kaeni mbali nacho! Msijiunge nacho! Ndicho alama ya mnyama, kaeni mbali nacho! Mnaona, Yesu anabisha katika wakati huu wa Laodikia. Mnaona mahali ambapo walimweka nje? Yeye anajaribu kuwafikia watu binafsi, sio—sio madhehebu na makundi ya watu. Anajaribu kumpata mmoja *hapa*, na mmoja *pale*, na mmoja *pale*, akijaribu. "Wote niwapendao, ninawarudi."

259 Kama vile maskini yule ndugu alivyokuwa na ono hapa, naye akasema alikuwa na ono. Na kusema, "Nuru ii hii mnayopokea, husababisha mauti yenu, pia." Mnaona?

260 "Wote niwapendao, ninawarudi; iweni na juhudi, na mrudi. Nasimama mlangoni, na kubisha." Sasa, angalieni, mafuta ya kuuni hayatalifaidi hili.

> Lakini kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
> Iliyotolewa kwenye vena za Imanueli,
> Ambapo wenye dhambi wakitumbukizwa
> chini ya furiko hilo,
> Wanapoteza mawaa yao yote ya dhambi zao.
>
> Yule mwizi aliyekuwa akifa alifurahia kuiona
> Ile Chemchemi katika siku zake;
> Hapo nijalie, ingawa ni mwovu kama yeye . . .

261 Yeye aliyafungua macho yangu, kwa dawa Yake ya macho. Roho Wake alishuka na kuiwasha moto Biblia, dawa Yake ya macho. Nisingeweza kuiona. Nilikuwa tu mchungaji wa Kibaptisti wa mtaani. Lakini siku moja alimtuma Roho Wake chini, hakuchemsha mafuta ya kuuni, bali alimtuma Roho Mtakatifu na moto! Dawa ndogo ya macho ikapakwa kwenye Biblia yangu—Biblia zangu. . . nami ningeweza kuona kwa jicho langu, ninamaanisha ikapakwa machoni mwangu kwa hiyo niliweza kuiona Biblia yangu. Nami nikaona ya kwamba, "Alikuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe ni kweli. Ninasimama mlangoni, na kubisha."

262 Hadithi moja ndogo tena. Je! tuna wakati? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naam, naam, ndipo nitaondoka, mnaona.

263 Kulikuwako na mzee mmoja mweusi huko chini Kusini. Na, mchungaji wake, nilimfahamu, maskini mzee mwema. Tulimwita Gabe. Jina lake lilikuwa ni Gabriel, nasi tulimwita tu Gabe. Yeye daima, mimi pamoja na mchungaji, tu—tulienda kuwinda, mara nyingi sana. Yeye alikuwa ni ndugu mweusi mzee, nasi tulitoka tukaenda kuwinda. Na kwa hiyo mzee Gabe alipenda kuwinda zaidi ya mtu yeyote niliyepata kumjua, bali hakuwa na shabaha. Kwa hiyo, siku moja yeye pamoja na mchungaji wake walienda kuwinda.

264 Wala kamwe tusingeweza kumfanya mzee Gabe ajiweke sawa na kanisa. Kamwe asingefanya hivyo. Asingekuja kanisani. Alisema, "A-ha, siyendi huko chini waliko wanafiki."

265 Nikasema, "Lakini, Gabe, mradi tu unakaa nje, wao ni wakubwa kuliko wewe. Unajificha nyuma yao, unaona." Nikasema, "Unajificha nyuma yao. Wewe ni mdogo kuliko walivyo wao; wanashuka wanaenda na kufanya jitihada, unaona."

266 Na kwa hiyo akasema, "Na—na—na—na—nakupenda sana, Bw. Bill. Lakini," kasema, "Ni—ni—ni—ninajua maskini Jones huenda huko chini, naye si kitu; yeye hucheza kamari, na yote hayo."

267 Nikasema, "Hiyo ni sawa, Gabe. Unaona, hiyo ni sawa. Lakini, kumbuka, Jones hana budi kuwajibika kwa jambo hilo; hutawajibika wewe, unaona. Kama ukienda tu. . . " Nikasema, "Mna mchungaji mzuri."

268 "Loo, Mchungaji Jones ni mmoja wa watu wazuri sana walioko humu nchini!"

269 Nikasema, "Acha awe ndiye mfano wako, endapo huwezi kuangalia mbele zaidi ya hapo. Acha awe ndiye mfano wako."

270 Kwa hiyo siku moja Ndugu Jones alisema, alimchukua mzee Gabe wakawinde, na akasema, "Tulipata sungura wengi zaidi

na ndege, siku hiyo, kuliko tungaliweza kubeba." Kisha kasema, "Ikafikia wakati wa jioni." Kasema, "Mzee Gabe alikuwa akifuata kwa nyuma, na wamelemewa sana na mzigo, unajua, namna hiyo." Na mkewe alikuwa Mkristo halisi, mwaminifu. Alikuwa na mahali pake pale pale, mwanamke aliyejazwa na Roho Mtakatifu, naye daima alikuwa anatekeleza wajibu wake. Kwa hiyo yeye alikuwa. . . Mzee Gabe alikuwa akifuata kwa nyuma, unajua. Ndipo Mchungaji Jones akasema aliangalia huku na huku, angeweza kuona, "Mzee Gabe alikaza kuangalia juu ya bega lake, namna *hiyo*. Jua lilikuwa likitua," kasema, "linashuka kabisa, baridi inaingia." Kasema, "Baada ya kitambo kidogo," kasema alikuwa akitembea, kasema, "mzee Gabe akamfikia. Alikuwa amening'inizia sungura na ndege tupu kwenye mtutu wa bunduki yake, na kadhalika." Kasema, "Akamgusa mchungaji begani, na kusema, 'Mchungaji?'"

Kasema, akageuka, kasema, "Naam, Gabe, kuna nini?"

271 Kwa hiyo akaangalia, na machozi makubwa yakitiririka mashavuni mwake meusi, ambapo ndevu zake zilikuwa zinaingia mvi. Akasema, "Mchungaji, mii nimekuwa nikitembea humu ufukoni, kwa karibu nusu saa." Kasema, "Nimekuwa nikiangalia hilo jua likishuka." Kasema, "Unajua, masharubu haya yangu yenye mvi, na nywele zangu zikiingia mvi," kasema, "unajua, jua langu linatua pia, mchungaji."

272 Kasema, "Hiyo ni kweli, Gabe." Na akasimama tu na kugeuka, kasema, "Una shida gani?"

273 Akasema, "Jua langu linatua, pia." Akasema, "Unajua nini?" Kasema, "Nilianza kuwaza," akasema, "nilipokuwa nikitembea kule nyuma." Akasema, "Unajua," kasema, "hapana budi Bwana ananipenda."

Kasema, "Hakika, Yeye anakupenda, Gabe."

274 Kasema, "Unajua, mimi sina shabaha." Kasema, "Nisingeweza kupiga chochote, lakini," kasema, "kweli tu—tulihitaji nyama hii nyumbani." Kisha akasema, "Hebu angalia tu lundo la wanyama wazuri wakubwa ambalo Yeye amenipa, hawa ndege na hawa sungura." Akasema, "Nina ya kutosha kutulisha sisi wote juma lijalo." Kasema, "Hapana budi alinipenda, maana siwezi kupiga chochote, unajua." Kasema, "Nisingeweza kumpiga, lakini hebu angalia kile Yeye amenipa." Ndipo akasema, "Hapana shaka Yeye ananipenda, la sivyo asingenipa hawa."

Kasema, "Hiyo ni kweli."

275 Basi akasema, "Vema, nilisikia mbisho mdogo wa kigeni mlangoni pangu, huko chini. Aliniambia nigeuke, kasema, 'Gabe, jua lako linatua, pia.'" Kasema, "Mchungaji, unajua nililofanya, mchungaji?" Akasema, "Nilimtolea ahadi."

276 Akasema, "Gabe, ninataka kukuuliza jambo fulani." Kasema, "Ni mahubiri gani niliyohubiri yaliyokufanya kujisikia jinsi hiyo?" Akasema, mchungaji, ama akasema, "Sasa ngoja kidogo," kasema, "ni—ni—ni kwaya gani iliyoimba?"

277 Akasema, "Loo, hakika ninapenda huo uimbaji huko chini kanisani, mchungaji." Akasema, "Ninapenda kila ujumbe unaohubiri, maana unatoka moja kwa moja kwenye Kitabu hicho kizuri, nami ninajua ni wa kweli. Lakini," kasema, "haikuwa ni hayo." Kasema, "Yeye alibisha tu, nami nikaangalia huku na huku hapa, na kuona jinsi alivyokuwa ni mwema kwangu, yale aliyonipa." Akasema, "Jumapili asubuhi, mii nitaenda moja kwa moja huko mbele mahali unaposimama." Akasema, "Nitakupa mkono wangu wa kuume," kasema, "kwa kuwa tayari nimempa Bwana moyo wangu, pale chini ya kile kilima pale." Akasema, "Mii nitabatizwa, na kupachukua mahali pangu papo hapo karibu na mke wangu. Nami nitakaa hapo mpaka Bwana atakaponiita juu zaidi." Unaona, ilitokea tu kwamba aliangalia huku na huku na kuona jinsi Mungu alivyokuwa mwema kwake.

278 Mimi ni mmishenari. Laiti mngaliweza kuangalia kwa macho ninayoangalilia sasa, na kuona mahali pa Mhindi, maskini hao watu wenye njaa, akina mama wakifa kwa njaa mtaani, maskini watoto wao wadogo hata hawawezi kulia tena, kutokana na njaa, na muwazie kile tulichokuwa nacho hapa leo hii. Myaangalie magari mliyokuja nayo. Muangalie nguo mnazovaa. Muangalie jinsi mlivyo matajiri. Ewe rafiki, hivi huwezi kusikia huo mbisho mdogo pale mahali fulani?

Hebu na tuombe.

279 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, na mioyo yetu, wakati dakika sasa zikipita mbio, karibu dakika saba ifike adhuhuri. Ndugu yangu, dada, sayansi inatwambia kwamba zimebaki chini ya dakika tatu ifike usiku wa manane. Sasa kama unaweza tu kuangalia huku na huku, na kuwaza tu kwa dakika moja. Watoto wako wadogo wameketi hapo karibu nawe. Ni maskini watoto wangapi wenye kifafa . . .

280 Mwangalie mke wako mzuri, ndugu, na uwazie ni wanaume wangapi ambao wana thamani ya mamilioni ya dola, naye anampenda mwanamke kwa moyo wake wote, naye ni kahaba wa baa. Yeye angetoa milioni yake baridi kumfanya mwanamke huyo ampende jinsi ambavyo mke wako anavyokupenda. Nawe, mke, ni wanawake wangapi . . .

281 Ni akina mama wangapi walio hapa asubuhi ya leo pamoja na watoto wao wadogo, ni akina baba wangapi; mbona, jamani, kuna wanaume wengi wanaoangalia kitanda cha mtoto, mtoto mdogo aliyekunjamana, maskini mtoto huyo, kiwete, na hebu angalieni jinsi mlivyo na watoto wadogo wazuri. Mnaona? Na wengi wenye umri mkubwa kidogo, pengine . . .

282 Ee Mungu! Kuna mambo mengi sana, kama tu ungeangalia. Yeye amekuwa mwema sana kwetu Wamarekani. Sasa hivi huwezi kujisikia kwamba ungetaka kupata dawa kidogo ya macho, asubuhi ya leo, "Yafungue macho yangu kidogo tu zaidi, Bwana, yafungue macho yangu"? Kama vile dada yetu alivyoimba vizuri sana, "Macho Yake yako kwenye shorewanda, shorewanda mdogo tu, nami ninajua Yeye ananiangalia."

283 Sasa anakuangalia moja kwa moja sasa. Hivi unaweza tu kusikia, chini mahali fulani, mbisho mdogo namna *hii*, [Ndugu Branham anagonga kitu fulani—Mh.], "Ninazuru, asubuhi ya leo"? Ndiyo heshima kubwa sana ingaliweza kutolewa, kama unaweza kuusikia mbisho huo moyoni mwako.

284 Hivi waweza tu kuuinua mkono wako, useme, "Kwa huu, Bwana, kwa msaada Wako na neema Yako, tangu leo na kuendelea, nitaishi karibu sana na Wewe nijuavyo kuishi. Hayo tu ndiyo ninayojua kukuomba"? Mungu akubariki. Mungu akubariki. "Kwa msaada Wako na neema Yako, leo hii, tangu leo na kuendelea, kamwe sitasahau jambo hili."

"Tazama, ninasimama mlangoni, na kubisha. Kama mtu yeyote . . . "

285 Sasa, kumbukeni, Yeye alikuwa akibisha wapi, kwenye hicho kibanda? La. Kwenye baa? La. Yeye anabisha wapi? Kanisani!

286 "Mtu yeyote akiisikia Sauti Yangu, na kunifungulia, nitaingia na kula pamoja naye, naye pamoja na Mimi."

287 Mungu mpendwa, maneno haya madogo yaliyovunjika-vunjika, yaliyochanganyika, machache ambayo yamenenwa asubuhi ya leo, kwa namna fulani jalia Roho Mtakatifu ayafasiri kwenye mioyo ya watu hawa.

288 Sasa kulikuwako na wengi, Bwana, labda kutoka kwenye hawa mia moja hapa kulikuwako na watu ishirini ama thelathini walioiinua mikono yao. Sina njia kabisa ya kujua walichotaka, Bwana. Lakini ninajua ya kwamba adhuhuri imesalia tu dakika chache, na vivyo hivyo na Kuja kwa Bwana; hata hivyo, kabla theluji hii haijayeyuka ardhini, huenda tukaitwa, na huenda huu ukawa ndio ule wakati ambao utabadilisha siku zote za usoni kuhusu kama wao wataachwa hapa ama wataenda juu.

289 Mungu mpenzi, kwa unyenyekevu tunamkubali Yesu, tunayakubali maneno Yake yote. Tujaze, Bwana, tujaze na Roho Wako Mtakatifu, kusudi maisha yetu yapate kuzaa tunda moja kwa moja. Tujalie, Bwana.

290 Tusamehe makosa yetu yaliyo mengi. Loo, tumejaa sana hayo, Bwana. Wala hatuna kitu tunachoweza kutoa, Bwana, maana, kila kitu tulicho nacho, Wewe ulitupa hicho. Kama vile Gabe alivyosema, katika hadithi hiyo ndogo tuliyosimulia sasa hivi, "Wewe, Wewe hakika unatupenda, Bwana, la sivyo usingefanya jambo hili." Na, kuwazia, watu hawa wameketi

hapa tangu mapema asubuhi hii, wameketi hapa tangu saa mbili, wameketi hapa kwa saa nne. Wanakupenda, Bwana. Wanakupenda. Sasa, Baba, naomba utume dawa ile ya macho ya Roho Mtakatifu, yafungue macho yetu. Tujalie . . .

291 Hawa walio humu mjini, jalia waende haraka kwenye ule uamsho usiku wa leo, jalia kuwe na umwagikaji mkuu! Tujalie, Bwana. Jalia uamsho wa mtindo wa kale uibuke hapa mjini. Lijalie. Mbariki kila mtu anayejitahidi, kila mmoja wa watumishi Wako kote ulimwenguni, ambaye anajitahidi. Kuwa pamoja nao, Bwana, na uwasaidie.

292 Yafungue macho yetu tupate kuona, zaidi na zaidi, mfano wa Kristo. Tujalie, Bwana. Tusamehe dhambi zetu.

293 Na sasa hawa walioinua mikono yao, Baba, ninawakabidhi Kwako. Wapokee. Sasa ninalinukuu Neno Lako Mwenyewe, Bwana, ambalo, "Mbingu na nchi zitashindwa, lakini," Wewe ulisema, "yeye," ambacho ni kiwakilishi nafsi, "yeye ayasikiaye Maneno Yangu . . ." Bwana, huenda yalikuwa yamevunjika-vunjika na ni rahisi, lakini mtu fulani aliyasikia. Mbegu ilianguka. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na," kiunganishi, "kumwamini Yeye aliyenipeleka," kwa kuwa alifanya jambo hili, "yuna (wakati uliopo) Uzima wa milele, wala katika siku za usoni hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Wao waliinua mikono yao, Bwana. Walivunja (kila) kanuni ya kisayansi; nguvu za uvutano huishikilia mikono yetu chini. Bali walithibitisha ya kwamba kuna roho fulani ndani yao, ambayo ingeweza kusikiliza mbisho mlangoni, nao wakainua mkono wao wa kuume kuelekea Mbinguni. Sasa fungua mlango. Fungua, Bwana, na uingie ndani. Sisi ni Wako. Tupokee, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

294 Je! mnampenda? Sijui kama tunaweza tu kuyafumba macho yetu, kwa dakika moja. Sasa kutoka mioyoni mwetu, huku tumeinua mikono yetu.

> Nampenda, nampenda kwa- . . .

295 Tunakubali mbisho Wako, asubuhi ya leo, Bwana. Mikono yangu imeinuliwa. Mikono yetu yote imeinuliwa, Bwana.

> Na . . .

Sasa ingia ndani, Bwana Yesu. Ingia mioyoni mwetu ukale pamoja nasi, nasi tutakula pamoja Nawe.

> Mtini Kalvari!

296 Je! mnampenda? Loo, nafikiri Yeye ni wa ajabu sana! Nanyi je? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hivi hamuusikii Uwepo Wake ukiwasugua-sugua tu? Ninajisikia kubarikiwa

sana sasa hivi, na—najisikia tu vizuri sana, jambo fulani kulihusu.

Imani yangu inakuangalia Wewe,
Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari,
Mungu Mwokozi;
Sasa nisikie niombapo,
Ondolea mbali dhambi zangu zote.
Ee nijalie tangu leo
Kuwa Wako kabisa!

297 Sasa ninawatakeni, tunapoivumisha aya hii nyingine ya wimbo huo mzuri wa dini, wimbo wa kale wa kanisa, ninakutaka upeane mikono na mtu fulani. Baki tu kwenye kiti chako, useme tu, "Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, dada. Nina furaha sana kuwa pamoja nawe hapa!" Hebu na tufanye hivyo. [Ndugu Branham pamoja na kusanyiko wanauvumisha, *Imani Yangu Inakuangalia*, na kupeana mikono mmoja kwa mwingine—Mh.] Mungu awabariki, Carl na Ndugu Williams. Nina furaha kuwa hapa.

298 Wazieni tu, mikono ya Mmethodisti iliishika ya Mpentekoste, ya Mbaptisti ikaishika ya Mpresbiteri.

Loo jalia . . . tangu leo
Niwe Wako kabisa!

299 Sasa tunapoimba polepole sasa, pia, kutoka kwenye kilindi cha moyo wako. Unajua, baada ya Ujumbe, unaosugua na kukemea, nafikiri ni vema kuingia katika Roho na kuimba, ule utamu wa Roho Mtakatifu.

300 "Tazama jinsi ilivyo vema ndugu wakae pamoja kwa umoja!" Biblia ilisema, "Ni kama mafuta ya kutiwa yaliyokuwa kwenye ndevu za Haruni, yaliyoshuka kwenye pindo za mavazi yake." Ninyi ni watu wazuri sana hapa. Ninatumaini kurudi kuwaona tena kabla Yesu hajaniita, ama ule Utawala wa Miaka Elfu. Nisiporudi, nitawaona ng'ambo ya mto huko ng'ambo. Nitakutana nanyi mtoni. Amina. Ni miadi.

Wakati nikitembea kwenye mzingile wenye giza,
Na huzuni imenizunguka,
Kuwa Kiongozi wangu;
Agiza giza ligeuke kuwa mchana, (hiyo Nuru ndogo wanayonena habari zake)
Pangusia mbali machozi ya hofu,
Ee nijalie tangu leo
Niwe Wako kabisa!

301 Kila mlango umefunguliwa! Loo, bonyeza tu kile kitufe kidogo, uone yote yakizunguka moja kwa moja kwenye duara; useme, "Karibu ndani, Bwana Yesu, kuwa Bwana wangu, yote kwangu."

Ee nijalie tangu leo, nisikuache usimame mlangoni,
Niwe Wako kabisa!

302 Ninyi mlioiinua mikono yenu na mnataka kuongozwa mbele zaidi kwa Bwana, ninawaomba mshuke mwende kwenye ule uamsho usiku wa leo. Nami nina hakika mchungaji wa huko atawachukua kotoka hapa mpaka kwenye ule mkahawa. Yeye ana mapeni sita, ama yoyote yaliyotolewa, kuwashughulikia, na divai na mafuta ya kumiminwa. Yeye anaweza kuimaliza kazi hii.

303 Mungu awabariki sasa. Nitairudisha ibada kwa, nadhani, Ndugu Williams, ama yeyote yule ambaye. . .

Milango Ndani Ya Mlango SWA65-0206

(Doors In Door)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi asubuhi, tarehe 6 Februari, 1965, kwa ajili ya kiamshakinywa cha Ushirika wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Hoteli ya Americana huko Flagstaff, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org